**BOT** kuondoa noti zamani mzunguko wa fedha

UKURASA 2



**NHC** yataka sera unafuu wa kodi kwa vifaa ujenzi

UKURASA 3

**Waziri** Mkuu aipa kibarua TAKUKURU ununuzi, ajira

UKURASA 3




# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Oktoba 27, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100

ISSN 0856 • No. 0581842

www.ippmedia.com

epaper.ippmedia.com

Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## KINACHOJIRI MITAANI

# Watoto wadogo wazagaa migahawa ya mamalishe

UKURASA 4



Mamalishe wakiendelea na shughuli zao katika mgahawa wao ulioko Stendi ya Zamani, Manispaa ya Tabora, huku wakiwa na watoto ambao wanaendelea na michezo katika eneo hilo. **PICHA: BENNY KINGSTON**

# IGP Wambura aonya watakaovuruga uchaguzi

UKURASA 2

## CHADEMA yakana uvumi kutoshiriki uchaguzi mitaa

UKURASA 3


**MICHEZO** FADLU APAGAWA VIWANGO WACHEZAJI WAKE UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Othman awafunda maadili wanasheria

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema Chama cha Wanasheria Zanzibar, kinapaswa kuwa kimbilio la wananchi pale haki zao zinapovunjwa.

Pia amesema chama hicho kinapaswa kuwa msatari wa mbele katika kupaza sauti za wananchi na kuwatetea.

Othman aliyasema hayo jana katika Hoteli ya Verde, Maruhubi mjini Zanzibar, alipofungua mkutano Mkuu wa Jumuiya ya Wanasheria Zanzibar, ambao pamoja na mambo mengine, utafanyika uchaguzi wa viongozi mbalimbali wa taasisi hiyo.

Alisema jumuiya hiyo ina wajibu, mbali na kupaza sauti haki za wananchi zinapovunjwa, kuchukua hatua stahiki kwa wanaohusika na uvunjaji wa haki hizo.

Makamu wa Kwanza wa Rais alisema chama hicho kinapaswa kuwa mlinzi namba moja wa Katiba ya nchi na mfumo wa utoaji haki, utawala wa sheria pamoja na demomkrasia.

Aliwaambia wanasheria hao kuwa wana wajibu wa kulinda haki za kiraia, kwa kuwa kazi mojawapo waliyo nayo ni kusimamia mashauri yenye maslahi na umma.

Kwa mujibu wa Othman, haipendezi pale haki za kiraia zinapokuwa hatarini ama kutokana na sababu ya wenye mamlaka au maslahi ya kibiashara, hivyo chama hicho kisikae kimya badala yake kitimize wajibu wake wa kupaza sauti kuutetea umma.

Alitoa wito kwa wanasheria kuendelea kujifunza, ili kukuza uwezo na ufanisi kwa kukabiliana vyema na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, kiuchumi na hata mwingiliano wa kijamii pamoja na matukio ya kihalifu ambayo hayakuzoelekea kusikika nchini.

Pia aliwataka wananasheria hao kutumia nafasi waliyo nayo katika kuchangia jitihada za kueleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia ushauri wao wa kisheria sambamba na kuhakikisha makubaliano na mikataba inazingatia vyema sheria, ili kuepuka migogoro.

Kuhusu uchumi wa Buluu, Othman alisema kuna fursa nyingi ikiwamo sekta ya mafuta na gesi asilia, sambamba na kulitumia vyema eneo la usafiri na usafirishaji wa anga, kwa kufuatilia fursa nyingi zilizoko na kujifunza ili kufaidika nao.

Aliwakumbusha wanasheria hao kuwa waadilifu wenye kufuata maadili ya taaluma na wananchi wapate fursa za kutumia haki zao bila vizuizi.

Waziri Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema jumuiya hiyo imekuwa msaada mkubwa kwa serikali na kwamba serikali itaendelea kujenga ushirikiano na taasisi hiyo.

Naye Rais wa Chama cha Wanasheria Zanzibar anayemaliza muda, Masoud Rukazibwa, alisema chama kinakabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwamo upungufu wa rasilimali hususan katika maeneo ya vijijini ambako huduma bado zinahitajika sana.



Ofisa wa Tigo, Abubakar Mahamba (kushoto), akizungumza na msanii wa filamu, Ayoub Kondo 'Black Jesus', kuhusu mkopo wa simu janja katika banda lililopo kwenye Tamasha la 43 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni (TaSUBa), mjini Bagamoyo, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UCHAGUZI UJAO

# IGP atoa onyo wavurugaji amani

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Nchini limesema katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwakani, halitavumilia mtu au kikundi cha watu kitakachovunja sheria kwa kisingizio chochote.

Limesema hatua za kisheria zitachukuliwa, ili jamii iendelee kuishi kwa amani na kutimiza haki ya kikatiba kushiriki uchaguzi huo.

Mkuu wa Jeshi hilo, Inspekta Jenerali (IGP) Camilus Wambura, aliyasema hayo jana wakati akifunga Mafunzo ya Awali ya Polisi Kozi Namba Moja ya Mwaka 2023/24 yaliyofanyika katika Shule ya Polisi Tanzania (CCP), Moshi mkoani Kilimanjaro.

IGP Wambura alisema Jeshi la Polisi pamoja na kutekeleza majukumu yake, lina wajibu wa kuhakikisha amani na utulivu vinatamalaki na askari wote wanadumisha amani na uzalendo kwa taifa, kwa kusimamia sheria na kanuni za uchaguzi.

"Tuwapinge wote wenye nia mbaya wasioitakia mema Tanzania. Tuwapinge wote wenye nia mbaya wanaoshabikia uhalifu au vitendo vya uvunjifu wa amani ambavyo vingi vinachochewa na itikadi za siasa chafu, kwa maslahi ya watu wachache walio katika jamii zetu," alisema.

IGP Wambura alisisitiza kuwa nchi iko salama na kwa kushirikiana na Watanzania wanadumisha amani, ili taifa kuwa kisiwa cha amani na kimbilio la wageni wote duniani.

Alisema wanaendelea kukabiliana na uhalifu wa kisasa kama vile uhalifu wa kupanga na unaovuka mipaka, ikiwamo biashara haramu usafirishaji binadamu, uhalifu mitandaoni na utakatishaji fedha.

"Uhalifu huu kwa kiasi kikubwa umetokana na utandawazi unaochagizwa na kasi ya ukuaji wa teknolojia.

Vilevile, kama jamii tunakabiliwa na uhalifu unatokana na mmomonyoko wa maadili, ikiwamo kuendekeza mila na desturi potofu, unyanyasaji na ukatili dhidi ya watoto," alisema.

Wambura alisema nchi imeendelea kukumbwa na mauaji kutokana na wivu wa mapenzi, kujichukulia sheria mkononi na kulipiza kisasi.

Alisema kutokana na changamoto hizo, Jeshi la Polisi linaendelea na jitihada za kubuni miradi mipya ya Polisi Jamii yenye dhumuni la kutokomeza mazalia na visababishi vya uhalifu kuanzia ngazi ya familia.

"Serikali imeendelea kuwekeza katika teknolojia ya kisasa ya kukabiliana na uhalifu wa kupangwa unaovuka mipaka, ikiwamo kudhibiti usalama wa mifumo ya kieletroniki na kudhibiti mipaka kwa mifumo ya kieletroniki na ongezeko kubwa la magari maalumu ya doria.

"Siri ya kutokomeza uhalifu ni kupanda mbegu wema ndani ya jamii na kuweka mikakati thabiti na shirikishi ya kukabili changamoto iliyoko na tumejipanga na tunaendelea kutoa elimu," alisisitiza.

IGP Wambura aliuhakikishia umma kuwa, wako imara na wametanua wigo wa ushirikiano na taasisi za serikali na zisizo za serikali, vyombo vya dini, wanasiasa na asasi za kiraia.

"Kidole kimoja hakivunji chawa. Mwanzilishi wa Jeshi la Polisi la kisasa alisema 'polisi ni jamii na jamii ni polisi' akimaanisha kila mwanajamii anao wajibu kushiriki katika juhudi za kushughulikia uhalifu na kuhakikisha amani na utulivu vinatamalaki katika taifa," alisema.

IGP Wambura alisema, ili kupunguza mzigo Jeshi la Polisi wa kupambana na uhalifu, wazazi na walezi hawana budi kuwalea watoto wao katika njia iwapasayo kwa kuwa uhalifu huanzia kwenye ngazi ya familia.

Kuhusu mafunzo hayo, alisema yamewajengea uwezo askari polisi wa kufanya kazi kwa weledi, ukakamavu na msisitizo wa nidhamu kwenye shughuli za polisi. Alisema shule imewafundisha na kuwachuja vizuri na sasa wanawapeleka vituoni kufanya kazi.

"Ili kutimiza vyema malengo ya kazi na kulinda raia na mali zao mkayaishi mliyofundishwa na kusimamia haki, kutenda kwa weledi na kuwa waadilifu na mkaishi kiapo mlichoapa na kutoa huduma bora kwa mteja," alisisitiza.

# BoT kuondoa kwenye mzunguko noti za zamani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imetangaza kuondoa noti mbalimbali za zamani kwenye mzunguko na kuwataka Watanzania kubadilisha kupitia ofisi za benki hiyo na benki za biashara kuanzia Januari, mwakani.

Noti hizo ni ya Sh. 20, 200, 500, 1000, 2000, 5000 na 10,000 kwa matoleo ya mwaka 1985 hadi 2003 na noti ya Sh. 500 iliyotolewa mwaka 2010 zenye sifa zilizoainishwa kwenye Tangazo la Serikali Namba 858 la Oktoba 11, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma na Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, ubadilishwaji unatarajiwa kuanza Januari 6 hadi Aprili 5, mwakani, kupitia ofisi za BoT na benki zote za biashara, kwa kupatiwa malipo yenye thamani sawa na kiasi kilichowasilishwa.

Aidha, alisema matumizi ya noti hizo yatafikia ukomo wa kuwa fedha halali za Tanzania kuanzia Aprili 6, 2025.

"Baada ya tarehe hiyo, mtu yeyote au taasisi yoyote inayomiliki fedha hizo haitaruhusiwa kuzitumia katika kufanya malipo popote duniani na benki hazitaruhusiwa kulipa wala kupokea amana au maombi ya kubadilisha noti zilizoondolewa kwenye mzunguko," alisema.

Alitoa rai kwa wananchi wote wenye akiba ya noti hizo kuzibadilisha au kuziwekea amana kwenye benki yoyote ndani ya muda huo.

HABARI KITAIFA

# Waziri Mkuu aipa kibarua TAKUKURU

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZIRI Mkuu, Kassimu Majaliwa, ametoa maagizo matatu kwa maofisa wapya uchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (TAKUKURU), akitaka wawe wakali katika mifumo ya ununuzi wa umma, utoaji wa ajira na ukusanyaji wa mapato.

Majaliwa aliyemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, aliyasema hayo jana mjini hapa katika Shule ya Polisi wakati wa kufunga mafunzo ya awali ya uchunguzi kwa maofisa 436 wa TAKUKURU.

Alisema katika maeneo hayo, bado kuna matatizo makubwa na kuwataka kutumia ujuzi walioupata pamoja na sheria, ili kutokomeza wala rushwa nchini.

"Ninyi si maofisa wa kukaa ofisini. Nendeni kwa wananchi, waelimisheni kuhusu rushwa na madhara yake. Watumieni wanasiasa wakiwamo madiwani na wabunge katika kuwapata wananchi. Tukatae rushwa.

"Wako watu wanaokosa huduma za afya, elimu na maji, hivyo ni wajibu wenu kuhakikisha rushwa inageuka historia hapa nchini," alisema.

Majaliwa aliitaka Wizara ya Elimu, Sanyansi na Technologia kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Miko na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuendelea kukamilisha mchakato wa usambazaji wa vitabu maalumu kwenye shule zote, ili somo la historia na maadili ya Mtanzania lianzie kufundishwa kuanzia mwanzoni mwa mwaka 2025.

"Sera mpya inaeleza lengo la serikali ni kujenga uzalendo na maadili ya nchi ikiwa ni sehemu ya kuchukia rushwa," alisema.

Majaliwa aliwataka kwenda kusimamia fedha zinazotolewa serikali katika miradi mbalimbali na kuwaainisha wala rushwa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Utumishi na Utawala Bora, George Simbachawene, aliwataka watumishi hao kufanya kazi itakayosaidia taifa.

"Mna bahati sana. Mliomba kazi, mmepata kazi. Kafanyeni kazi eneo lolote mlilopangwa, kawajibikeni na mlete mabadiliko," aliagiza.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Crispin Chalamila, alisema serikali imeendelea kuboresha vitendea kazi katika taasisi hiyo na kwa sasa watafanya kazi kwa weledi mkubwa na hawatakuwa na kisingizio chochote.

Chamamila alisema serikali imeshatoa Sh. bilioni 30 kwa ajili ya ununuzi wa magari mapya 195 na hadi sasa yameshanunuliwa magari 88 yatakayosambazwa katika ofisi mbalimbali za TAKUKURU wilaya na mikoa nchini.



Vijana wakijaribu kunyanyua mtambo kuuhamisha ulipo, bila kutumia kifaa maalum cha kunyanyulia, Tegeta, Dar es Salaam, jana. **Picha: JUMANNE JUMA**

# CHADEMA yakanusha uvumi kutoshiriki uchaguzi mitaa

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimekanusha taarifa zilizosanmbaa mtandaoni kuwa kimejitoa katika Uchaguzi Serikali za Mitaa na kusisitiza hakina mpango huo.

Sambamban a kuweka msimamo huo, chama hicho kimesema kimejipanga vizuri kushiriki na kushinda katika uchaguzi huo.

Jana, chama hicho kilianza kutoa fomu za serikali kwa wanachama wake walioteuliwa nchi nzima za kugombea nafasi mbalimbali waliozoteuliwa na chama.

Akizungumza jana na vyombo vya habari kuhusu uchaguzi huo, Spika wa Bunge la Wananchi wa CHADEMA, Suzan Lyimo, alisema chama hicho hakijajitoa katika kinyang'anyiro hicho kama uzushi uliosambaa mtandaoni.

Juzi, Mkurugenzi wa Itikadi, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, kupitia taarifa yao kwa umma, alisema hawajajitoa na wala hawana mpango wa kujitoa kwa sasa.

"Tunawahimiza wanachama wetu walioteuliwa nchi nzima kesho (jana) wajitokeze mapema kwenda kuchukua fomu za serikali za kugombea nafasi mbalimbali walizoteuliwa na chama," alisema.

Mrema alisema taarifa ya picha mjongeo iliyosambaa mitandaoni yenye maudhui kuwa CHADEMA imejitoa katika uchaguzi 2024, ni za uongo, uzushi na za kupuuzwa.

Katika mkutano huo, Lyimo aliendelea kusisitiza madai kwamba wameshuhudia mawakala kuzuia kupata takwimu za waandikishwaji na baadhi wakipingwa na wanafunzi chini ya miaka 18 wakishangaa kuandikwa.

Mwachumu Kadutu, Msemaji wa CHADEMA Ofisi ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (Tamisemi) kwenye Bunge la Wananchi, alisema upungufu waliouona katika mchakato uliofanyika kwa siku 10 hadi ubandikaji majina ni pamoja na waliyoona kwenye daftari lenyewe haviulizi ni raia wa wapi.

Alisema kilichofanyika ni mtu kuulizwa majina matatu, umri na kutia saini, kwamba hali hiyo inafungua mwanya hasa kwa mipakani wasio raia kushiriki mchakato huo.

"Haliulizi unakaa mtaa gani, inatoa mwanya kwa watu kutoka mtaa mwingine kwenda mwingine kupiga kura. Umri umetajwa miaka 18 kuendelea, lakini utathibitishaje kama ana umri huo? Ikitokea utamzuia," alihoji.

Alisisitiza madai kwamba wameshuhudia mapungufu ya wanafunzi kuandikishwa walio chini ya miaka 18 wakati kanuni inasema ni miaka 18 kuendelea.

"Vituo vingi vipo shule za sekondari, kwa kidato cha kwanza hadi kidato cha nne wameandikishwa, ukipiga hesabu mtoto mwenye umri wa miaka saba ambaye yupo kidato cha nne maana yake hajafikia kigezo cha kuandikishwa.

"CHADEMA tunaomba turuhusiwe kupiga kampeni shuleni wanahaki ya kusikiliza sera zetu kwa sababu wana haki ya kupiga kura, ili wanapochagua wachague kwa kusikia na kuona wagombea na kuelewa sera zao," alisema.

# NHC yataka sera unafuu kodi vifaa ujenzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC), limetoa mapendekezo kwa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC), kushawishi sera inayoleta unafuu wa kodi katika vifaa vya ujenzi na kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa wanunuzi, ili kuchochea Watanzania wengi kumiliki nyumba.

Wakati NHC ikitoa ombi hilo, Kamati imetoa tahadhari kwa serikali na kuitaka kuweka usimamizi wa majengo yake katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini hapa, ili yadumu kwa muda mrefu.

Mapendekezo hayo yalitolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Hamad Abdallah, wakati wa ziara ya kamati hiyo ya kukagua miradi nane ya majengo ya wizara yanayojengwa shirika hilo, kwa gharama za Sh. bilioni 186.8 katika mji huo na kutarajiwa kukamilika Januari 31, mwakani.

Akizungumza katika kikao cha majumuisho, Abdallah alisema shirika linatambua serikali ilishaanza jitihada za kuondoa VAT katika mauzo ya nyumba zilizo chini ya Sh. milioni 50, lakini wanaona ili sekta ya nyumba iwe na ustawi mkubwa, kodi hiyo iondolewe kwa wanunuzi wote.

"Wanunuzi wa nyumba za NHC ambao ni mmoja mmoja hawawezi kurejesha VAT kwa sababu hawafanyi biashara, mwaka jana serikali ilifanya uamuzi mzuri kwa nyumba zote ambazo thamani yake haizidi Sh. milioni 50 zinaondolewa VAT na hilo linafanyika.

"Lakini sisi tuna kiu ya kuona walau wanunuzi wote wa nyumba waondolewe hiyo kodi, kwa kuwa shirika litakuwa limelipa kodi zote za serikali zinazohitajika, ili kuwafanya Watanzania wamudu kulipa fedha zinazohitajika katika ununuzi wa nyumba, "alisema.

Alisema kwa sasa serikali imefanya vizuri kwenye sekta ya kilimo na mikopo yao ni kwa riba ndogo na kupendekeza kamati iishauri serikali kuangalia namna ya kuwawezesha Watanzania wanaochukua mikopo ya nyumba, wapate kwa riba ndogo.

"Haya yote tumewasilisha kwa kamati wameyabeba kwa kuwa mengine ni ya kisera, ili kuangalia ni kwa kiwango gani riba zitapungua ina Watanzania waondokane na upangaji waingie katika umiliki wa nyumba," alisema.

Alisema mahitaji ya nyumba kwa mwaka ni 200,000, hivyo ni muhimu kuwa na mkakati wa kupunguza uhitaji huo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Augustine Vuma, alisema kamati imeridhishwa na kasi ya ujenzi wa majengo hayo ambayo NHC ni mkandarasi na kusisitiza ikamilike kwa wakati uliopangwa.

"Tumeona majengo mengi hatua za ujenzi zipo zaidi ya asilimia 80 na wapo ndani ya mkataba waliowekewa, tunaamini watakamilisha ndani ya muda uliopangwa.

"Miradi hii itaipa nguvu NHC ijiendeshe kwa tija zaidi, ninaipongeza bodi kwa usimamizi mzuri wa shirika hili ambalo tunaona limefanya mageuzi makubwa yenye tija,"alisema.

Kuhusu utunzaji wa majengo, Mwenyekiti huyo alisema serikali imewekeza fedha nyingi katika ujenzi wa majengo katika mji huo na yapo mbioni kukamilika, hivyo ni vyema kuangalia namna ya kuyatunza vizuri.

"Huu mji kwa sasa unang'aa na serikali imetumia mabilioni kuujenga, baada ya muda fulani utakutana na uchakavu majengo yatakuwa hayang'ai kama yanavyong'ara kwa sasa.

"Majengo mengi ya serikali yamekuwa yakijengwa na kukamilika vizuri, baada ya muda ukienda unakuta miundombinu yote ya maji, majitaka na mwonekano wa jengo inakuwa changamoto," alisema.

KINACHOJIRI MITAANI

# Watoto wadogo watapakaa migahawa ya mamalishe

**Na Waandishi Wetu**



Mamalishe anayejulikana kwa jina la Mama Anna, akiwa na watoto wake kwenye mgahawa wake eneo la Ng'ambo, Mmanispaa ya Tabora wakishiriki kuchambua mboga za majani zinazoandaliwa kwa ajili ya kupikwa mgahawani hapo hapo. hao. **PICHA: BENNY KINGSTON**

FIKIRIA mtoto mwenye umri wa kwenda shuleni, badala ya kuwa darasani au nyumbani akijisomea, yuko mtaani akipita mitaa kwa mtaa kuomba fedha za michango kwa ajili ya ujenzi wa makanisa, misikiti au ununuzi wa gari la mchungaji.

Ni maisha ya kila siku ya watoto wenye umri wa kuwa shuleni, kabla au baada ya masomo kukutwa katika mitaa mbalimbali wakiwa na karatasi mkononi lenye jina la taasisi fulani, wakisimamisha watu barabarani kuomba fedha za michango.

Hayo yanafanyika wakati Sheria ya Mtoto Sura Namba 13 Toleo la 2014, Kifungu (a) namba 12, kikizuia mtu yeyote kumwajiri au kumfanyisha mtoto kazi ambazo zinaweza kuwa na madhara kwa afya, elimu, akili, mwili au kwa maendeleo ya kimaadili ya mtoto.

Kifungu hicho kikisomwa pamoja na namba 14 kuhusu adhabu, kinaeleza kuwa mtu atakayekiuka kifungu chochote katika sehemu hiyo, atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atalipa faini isiyozidi Sh. milioni tano au kifungo cha miezi isiyozidi sita au vyote kwa pamoja.

Katika mahojiano maalum na waandishi wa habari hii yaliyofanyika maeneo tofauti katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, baadhi ya watoto wamekiri kufanyika kazi hiyo.

**WATOTO WANENA**

Mtoto X, mkazi wa jijini Mwanza na mwanafunzi wa darasa la sita katika shule ya Msingi Igelegele, anasimulia kwamba wanapatiwa fomu za michango kanisani ili kuchangisha fedha mitaani kwa ajili ya ujenzi wa kanisa na wakati mwingine kukiwa na shughuli zingine za kimaendeleo.

"Mara nyingi tunapewa fomu hizo wakati wa mafundisho na unapopewa huwezi kukataa kwani ni maelekezo ya mwalimu ambaye anasema ni mpango iliowekwa na uongozi wa kanisa ili kufikia malengo ya ujenzi husika. Mara nyingi tunazunguka wengine huchanga na wengine hukataa," anasema.

Mwanafunzi wa Kidato cha Kwanza (jina linahifadhiwa) katika Shule ya Sekondari ya Ngara, anakiri kupewa fomu ya kuchangisha kwa ajili ya kwenda kwenye maombi nje ya mkoa.

Anasema pamoja na kupewa fomu hiyo, mwalimu wao wa dini huwa anawaelekeza mahali pa kwenda kuchangisha michango hiyo ikiwa ni pamoja na kanisani, kwa ndugu zao wa karibu na rafiki.

Mwanafunzi mwingine wa kidato cha tatu shuleni hapo (jina linahifadhiwa), anasema alipewa fomu na mwalimu wa malezi wa dini ili kuchangisha mtaani fedha za kongamano la kitaifa.

Anasema jukumu hilo halimwathiri kielimu kwa kuwa anatumia muda wake ipasavyo kukusanya michango na kisha kuendelea na masomo.

**WAZAZI WAFUNGUKA**

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, baadhi ya wazazi wamesema vitendo hivyo vinatweza utu wa watoto hao kutokana na kuzunguka maeneo mbalimbali wakiomba fedha bila kujali hali yao na hatari wawapo mitaani ambako magari, bajaji na pikipiki hupita.

Mkazi wa Ihayabuyaga Magu, mkoani Mwanza, Sara Tito, ambaye pia ni msusi, anakiri katika eneo lake la kazi kupokea watoto wa namna hiyo na kwa kwa wiki hupokea wastani wa watoto watatu.

Anasema mara nyingi wanapita na fomu za michango ya sherehe za kwaya, ujenzi wa makanisa na misikiti, huku wengine wakitumwa na wanaodaiwa kuwa wazazi, kutafuta fedha za matibabu kwa watoto wenzao.

"Saluni kwangu mara kwa mara wanapita, wengine wanahitaji michango ya mahafali, na ujenzi wa makanisa. Kama juzi alipitia mtoto akiomba mchango wa mtoto kuwa yuko hospitalini anahitaji matibabu. Kwangu mimi naona si sahihi kuwatumia watoto kwenye shughuli hizi," anasema.

Mkazi wa jijini Mwanza, Emmanuel Kido, anasema katika biashara yake ya duka, amekuwa akiwapokea watoto mara nyingi wakiomba kuchangiwa ujenzi wa misikiti, makanisa na vyumba vya madarasa na michango ya mahafali huku wakitaja baadhi ya viongozi wa maeneo husika kuwatuma wakiwa na ushahidi wa mihuri katika fomu zao.

Naye mkazi wa Mtaa wa Bariadi, Manispaa ya Kahama, Agatha Juma, anasema kuna watoto wengi mitaani wenye umri wa kwenda shuleni lakini wanatembea na fomu za kuomba michango ya ujenzi wa makanisa, ununuzi wa gari la mchungaji na mahafali, jambo ambalo ni kudhalilisha madhehebu na utu wa watoto husika.

Anasema huenda viongozi wa madhehebu hayo hawafahamu na badala yake kunaibuka kikundi cha watu wachache ndani ya makanisa na misikiti kinawatumia watoto kujipatia fedha, na kuwataka viongozi hao kuangalia namna ya kudhibiti suala hilo, lisiendelee kujitokeza katika jamii.

Mkazi wa Nyihogo, Zabroni Allex, anasema kuna wakati amekuwa huwakamata na kuwahoji wanapata wapi muda wa kwenda shuleni, kujisomea na wengi huzunguka mitaani kipindi cha mapumziko na wakati wametoka shuleni jioni.

Merania Marashi, mkazi wa Kata ya Mahina, Mwanza, anasema suala hilo linakera. Kila siku watoto wakitoka shuleni wakishakula huenda mitaani kuchangisha fedha, wengine wakidai kutumwa shuleni, makanisani na misikitini.

"Kila siku tunakemea ukatili majumbani. Lakini makanisani, misikitini huko nako kumekuwa chanzo cha ukatili. Unapomtuma mtoto mitaani akachangishe fedha unategemea nini?

"Kama si kutengeneza kizazi ambacho kitakuja kuwa hatari kwa taifa, maana uadilifu hautokuwapo kutokana na watoto kujua matumizi ya fedha wakiwa bado wadogo na wakati mwingine, kukutana na vishawishi huko mitaani," anasema Marashi.

**VIONGOZI WA DINI**

Baadhi ya viongozi wa dini pamoja na serikali waliotafutwa kuelezea suala hilo wanasema suala hilo sio la kiungwana na kuwakemea wanaofanya hivyo ya kuwa wanakiuka sheria ya mtoto.

Mchungaji wa Kanisa la Anglikana, wilayani Kahama, Esron Yuda, anasema ni kosa kuwatumia watoto katika kukusanya michango ya aina yoyote mitaani na kuahidi kulisemea jambo hili kanisani hasa siku za ibada, ili kama lipo walikemee lisiendelee kujitokeza, kwani linadharirisha imani zao.

Shekhe wa Wilaya ya Kahama, Alhaji Omary Damka anasema, wanapohitaji michango ya kuendeleza dini huwa wanatumia kamati maalum ambazo huandaliwa kwa ajili ya kukusanya michango na si kutumia watoto.

Anasema maendeleo yanohitaji kushirikisha jamii lakini si kwa kutumia watoto kupita mitaani kuchangisha fedha.

"Watoto wanahitaji uangalizi katika malezi, kuhimizwa kusoma kwa ajili ya maisha ya baadaye na husaidia kutojiingiza katika vitendo viovu," anasema.

Mwanasheria ambaye pia ni Kaimu Katibu Mkuu wa Shirika la Kutetea Haki za Binadamu (SHIHABI), Onesmo Daudi, anasema si sahihi kwa watoto kutumika kutafuta michango ya ujenzi wa makanisa na ununuzi wa magari ya wachungaji wao.

Anasema mzazi, mlezi au taasisi yoyote ya kidini hairuhusiwi kumbebesha majukumu mtoto kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009 na endapo atabainika atachukuliwa hatua za kisheria, hivyo majukumu yanamnyima mtoto fursa ya kwenda shule kusoma.

Daudi anasema wanalaani vitendo vya namna hiyo kwa kuwa hali hiyo mara nyingi imekuwa ikijitokeza katika madhehebu yanayochipukia.

Anawasihi wenyeviti wa serikali za mitaa kuwachukulia hatua viongozi wa dini wanabainika kuwatumikisha watoto.

Ofisa Elimu Wilaya ya Ngara, James John, anasema ofisi yake haijapokea taarifa zozote za wanafunzi kushiriki katika kukusanya michango hiyo wakati wa masomo na kuwa, kama litakuwa linafanyika ni nje ya muda wa masomo wakati wa likizo au baada ya kutoka masomoni, wakiwa mikononi mwa wazazi.

John anakemea vitendo hivyo na kueleza kuwa mtoto anatakiwa kupata nafasi ya kupumzika na kutafakali aliyojifunza shuleni na siyo kushiriki katika kusambaza fomu za michango ya namna hiyo.

- **Imeandaliwa na Shaban Njia (KAHAMA), Rose Jacob (MWANZA), Neema Emmanuel (MWANZA), Vitus Audax (MWANZA), Judith Julius (NGARA)**




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akipata maelezo kutoka kwa Christina Lucas wa Kampuni ya Fishermen Tours & Travel Ltd, alipotembelea maonesho ya Tamasha la Utalii na Uwekezaji Zanzibar 2024, linalofanyika katika viwanja vya maonesho Dimani Nyamazi, Wilaya ya Magharibi B, Unguja, jana. **PICHA: IKULU**

# ARGeo-C10 kuchochea ubunifu, uendelezaji wa nishati jotoardhi

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Shaibu Hamis Kaduara (pichani), amesema Kongamano la Kimataifa la Jotoardhi Afrika (ARGeo-C10), lililofanyika nchini kuanzia Oktoba 21, mwaka huu, litaleta uwekezaji na ubunifu mpya katika uendelezaji wa nishati ya jotoardhi.

Kaduara aliyasema hayo wakati hafla ya ufungaji wa kongamano hilo, lililofanyika jijini Dar es Salaam, juzi,

"Maarifa na utaalam uliopatikana katika kongamano hili, utasaidia muhstakabali wa Tanzania na Afrika katika kufikia suluhisho la upatikanaji wa nishati safi, kuongeza kasi ya maendeleo ya jotoardhi Tanzania na mchango wa nishati jadidifu katika uzalishaji umeme," alisema.

Alisema Tanzania imepata heshima kubwa, baada ya kuandaa kongamano hilo kwa mafanikio na imekuwa ni fursa ya kutangaza maeneo yake yanayohitaji uendelezaji, ikiwamo eneo la ngozi mkoani Mbeya ambapo kunachimbwa visima vitatu vya uhakiki wa mashapo ya jotoardhi.

Alisema kwa kuandaa kongamano la ARGeo-C10 Tanzania, imeonesha kwa vitendo nia yake ya kuendeleza jotoardhi, kushiriki katika biashara ya hewa ukaa na kutokuwa na uzalishaji wa hewa ya ukaa.

Kaduara aliwasihi washirika wa maendeleo duniani kuendelea kuunga mkono jitihada za kukuza nishati ya jotoardhi barani Afrika.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dk. James Mataragio, alisema kongamano hilo limefanikiwa kwa kiasi kikubwa, kwani nchi 14 ambazo ni wanachama wa Shirikisho la Jotoardhi Afrika zimeshiriki pamoja na nchi nyinginezo zipatazo 12.

Alisema limehusisha wataalam wabobezi kutoka mataifa hayo 26, ambao wametoa mafunzo maalum katika jotoardhi, ikiwamo masuala ya tathmini ya jotoardhi na namna ya nishati hiyo itakavyosaidia kuangalia masoko ya hewa ya ukaa.

Mataragio alisema kupitia kongamano hilo, nchi nyingi zimeonesha nia ya kuwekeza Tanzania, baada ya kuona utajiri wa jotoardhi uliopo na utayari wake katika kushirikiana na nchi nyingine duniani, ili kuiendeleza.

Mwakilishi wa Spika wa Bunge, Dk. Joseph Mhagama, alisema kongamano hilo limewawezesha wabunge walioshiriki kupata uelewa kuhusu masuala mbalimbali, ikiwamo matumizi ya moja kwa moja ya jotoardhi, fursa, changamoto na biashara ya hewa ukaa, hivyo uelewa huo utawasaidia kutoa ushauri kwa serikali na kuisimamia sekta ya jotoardhi kwa ujumla.

Mkuu wa Ofisi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Mazingira Duniani (UNEP) katika nchi za Kusini mwa Afrika, Meseret Teklemarian, alishukuru serikali kwa kuendesha kongamano la ARGeo-10 kwa mafanikio makubwa, huku likipewa msukumo mkubwa na kuahidi wao kuendelea kuiunga mkono Tanzania kwa namna mbalimbali, ili kuendeleza nishati ya jotoardhi.



Dk. Peter Omenda, Rais wa Shirikisho la Jotoardhi Afrika (AGA), alipongeza Tanzania kwa kujitoa ipasavyo katika kuhakikisha kuwa kongamano hilo linafanikiwa na kueleza kuwa, linalofuata linatarajia kufanyika Comoro mwaka 2026.

Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mathew Mwangomba, alisema Tanzania ipo tayari kushirikiana na wadau wengine, ili kuendeleza jotoardhi kupitia utaalam na uwekezaji kwenye maeneo yenye mashapo ya jotoardhi.

# SMZ yaahidi kuboresha mazingira biashara

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imesema itaendelea kukuza mazingira rafiki ya biashara na uwekezaji na kuweka mkazo wa kurahisisha michakato, kuimarisha mifumo ya udhibiti na kutoa motisha za kuvutia uwekezaji.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo alipofungua Maonesho ya Utalii na Uwekezaji Zanzibar, viwanja vya maonesho ya Biashara Nyamanzi, wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi, ikiwa ni mwendelezo wa kupongeza mafanikio ya miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya nane anayoiongoza.

Alisema Zanzibar imefungua milango wazi kwa fursa za biashara na uwekezaji na tayari imewakaribisha wadau mbalimbali, kushirikiana nao kwenye maono ya ukuaji wa Uuchumi endelevu na ustawi wa utalii wa muda mrefu.

Dk. Mwinyi alisema maonesho hayo yamedhihirisha thamani ya ushirikiano baina ya wadau wa utalii nchini, Sekta ya Umma na Kibinafsi (PPP) na kwamba ushirikiano wao ni njia muhimu za kufikia malengo ya pamoja.

Rais Dk. Mwinyi aliwashauri wadau wa utalii kuendeleza utamaduni na shauku ya kufanya Maonesho ya Utalii na Uwekezaji si kwa mnasaba wa Zanzibar pekee, bali kwa Afrika Mashariki na medani za kimataifa, ili kuendelea kuitangaza nchi na vivutio vyake duniani kote. Alisema hatua hiyo itaiwezesha Zanzibar kuwa kituo bora cha ushindani kwa utalii kwenye ramani ya dunia.

Pia alisema maonesho hayo ni fursa nzuri za kubadilishana uzoefu, kuweka harambee, misingi ya miradi ya kuleta mabadiliko kwenye sekta ya utalii nchini na kuwahimiza wadau wa utalii kushiriki kikamilifu na kuchangia katika kuunda mustakabali wa utalii na uwekezaji Zanzibar.

Alisema maonesho hayo yanaashiria mwanzo wa mashirikiano mapya na wa kudumu na ubunifu tu si dhamira ya utalii na uwekezaji peke bali ari ya pamoja ya kuhakikisha kuwa Zanzibar inakuwa kinara wa ukuaji endelevu, uhifadhi wa utamaduni na maendeleo ya kiuchumi.

Katika hatua nyingine, Rais Mwinyi alisema sekta ya utalii licha ya kuwa ni uti wa mgongo wa uchumi, bado inaakisi nadharia nzima ya maisha ya Wazanzibari, elimu kwa vizazi vilivyopo pamoja na kuhifadhi utamaduni wa utambulisho wa taifa.

Dk. Mwinyi alibainisha kwamba faida za utalii na uwekezaji zinufaishe visiwa vyote vya Unguja na Pemba, kwa kutengeneza fursa kwa watu wote.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrick Ramadhan Soraga, alipongeza juhudi za maendeleo zinazofanywa na Rais. Mwinyi kwamba mafanikio makubwa yaliyopo kwenye sekta ya utalii ni kazi kubwa inayofanywa na kiongozi huyo.

Pia alisema miaka minne ya mafaniko kwenye uongozi wa Dk. Mwinyi, imeakisi maendeleo endelevu ya sekta ya utalii na kukuza biashara na uwekezaji nchini.

Maonesho hayo ya Utalii na uwekezaji Zanzibar, 2024 yameandaliwa kwa ushirikiano na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Kamisheni ya Utalii na sekta binafsi.

Katika hafla hiyo pia kulitiwa saini makubaliano ya ushirikiano baina ya Kamisheni ya Utalii Zanzibar na Mamlaka ya Uwekezaji na Vitegauchumi Zanzibar (ZIPA) katika kuendeleza kazi za utalii na kurahisisha uwekezaji kwa kuendeleza vivutio vipya kwa maeneo ya utalii nchini.

Aidha, yalitiwa saini makubaliano baina ya Kamisheni ya Utalii Zanzibar na Baraza la Sanaa Zanzibar katika kuondosha changamoto zinazotokana na utalii, hususan eneo muziki, sanaa na burudani.

Rais w
sein A
maele
tina L
Fishe
Ltd, a
sho y
Uwek
linalo
vya m
amaz
ibi B,
**IKULU**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua zichukuliwe kuwaokoa watoto katika majanga haya

**KATIKA** ukurasa wa ne wa gazeti hili, kuna ripoti maalum inayoeleza kuzagaa kwa watoto kwenye migahawa ya mamalishe katika miji mbalimbali, huku Manispaa ya Tabora na jiji la Mwanza ikiwa mfano.

Watoto hao si kwamba hawana wazazi bali ni wa mamalishe hao ambao wamedai kuwa wanakwenda nao katika maeneo ya kujipatia riziki kutokana na kukosa wasichana wa kuwaachia. Kutokana na sababu hiyo, wameeleza kuwa suluhisho walilolіona ni kwenda nao katika shughuli za kila siku.

Licha ya sababu hiyo, mamalishe hao wamesema wanalazimika kufanya hivyo, kwa sababu ya hali ya kipato chao kushindwa kuajiri watumishi wa ndani kwa ajili ya kulea watoto hao. Pia mmoja amesema sababu ya kufanya hivyo ni kutokana na mwenza wake kushindwa kuwajibika kwa matunzo ya familia na kwamba yeye ndiye mtafuta riziki ndani ya ndoa yao.

Picha zilizopigwa katika maeneo hayo zinaonesha kuwa mazingira wanayokuwa watoto hao katika migahawa ya mamalishe si rafiki, kwa makuzi yao wala afya kwa ujumla. Watoto hao wameonekana wakichambua mboga, wakicheza katika maeneo hatarishi yakiwamo maegesho ya magari.

Kulingana na mazingira hayo, watoto hao ni rahisi kuchukua tabia na matendo yanayofanyika kwenye maeneo hayo kama vile matusi na udhalilishaji.

Kwa mantiki hiyo, kama inavyofahamika, kuna uwezekano mkubwa mustakabali wa watoto hao ukawa mbaya kwa kuwa mtoto ana tabia ya kunakili, kuiga na kuchukua kila kitu kinachofanyika katika mazingira husika. Kwa hiyo, kuna uwezekano mkubwa watoto hao wakajikuta wanakua na kuishi katika mazingira ya matusi, huku wakishuhudia kauli chafu kutoka kwa wateja wa mama zao.

Baadhi ya viongozi, wakiwamo watendaji wa kata na mitaa, wamekiri kufahamu vitendo hivyo na kwamba wanatarajia kuchukua hatua dhidi ya wazazi, ili kuwalinda watoto na mazingira magumu waliyomo. Lakini jambo la kujiuliza walikuwa wapi mpaka kutamka kuwa wnatarajia kuchukua hatua ilhali jambo hilo limeshaota mizizi?

Ni dhahiri kwamba kwa muda ambao watoto hao wameshakaa katika mazingira hayo, tayari kuna athari za kisaikolojia, kiafya na makuzi ambazo wameshazipata. Pamoja na hayo, kama waswahili wasemavyo kawia ufike, bado kuna nafasi ya kuwaokoa watoto hao dhidi ya majanga yanayoweza kuendelea kuwakumba kama wataendelea kuwamo katika mazingira hayo.

Serikali za mitaa, kupitia watendaji wa kata na mitaa pamoja na wataalamu wa elimu, afya na mazingira, wanapaswa kuchukua hatua za haraka kuwanusuru watoto hao, ambao miaka mingi wamekuwa wakitajwa kuwa ndio taifa la kesho. Mpango mmojawapo unaoweza kufanyika ni kuwapeleka katika shule za awali zilizo karibu na mamalishe hao na kuchukuliwa, baada ya mama zao kumaliza shughuli zao.

Njia nyingine inayoweza kuchukuliwa na kuwanusuru ni kuweka sheria ndogo katika mamlaka za serikali za mitaa zitakazowazuia wazazi kwenda na watoto wao kwenye shughuli zao za kujipatia riziki kama vile migahawa ya mamalishe. Aidha, iko sheria inayomlinda mtoto, hivyo nayo inapaswa kutumika, ili watoto hao waokolewe dhidi ya madhila yanayowanyemelea.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, mzazi atakayemweka mtoto katika mazingira hatarishi anaweza kufikishwa mbele ya sheria na kutozwa faini au kifungo, au kupewa adhabu zote kwa pamoja.

Ni imani kwamba kama sheria hizo zitatekelezwa, kutakuwa na fundisho kubwa dhidi ya wazazi kama hao na wakati huo huo, watoto kuokolewa kwenye majanga yanayowakabili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tujipange kuchagua viongozi bora, si bora viongozi

Na Sabato Kasika

**MCHAKATO** wa kujiandikisha katika daftari la makazi, kwa ajili ya uchaguzi wa viongozi wa vitongoji, vijiji na mitaa, ulimalizika Oktoba 20, mwaka huu. Kinachoendelea sasa ni kura za maoni ndani ya vyama.

Kura hizo ni kwa ajili ya kupitisha wagombea watakaochuana katika kinyang'anyiro cha uchaguzi wa viomgozi wa serikali za mitaa, unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu.

Kimsingi, suala la kujiandikisha kwa ajili ya kupigakura ni wajibu wa kila Mtanzania, aliyetimiza umri wa miaka 18 na kuendelea, kwa ajili ya kupata wawakilishi wanaotakiwa na umma. Kwa hiyo kwa sasa tunapaswa kujielekeza zaidi katika mchakato mzima wa sehemu muhimu kuhakikisha kwamba, tunaweka kipaumbele chetu zaidi cha kutambua nia, malengo, tabia na uelewa wa watiania katika nafasi hii ya kisiasa ya wenyeviti wa vitongoji, vijiji na mitaa.

Huu ndio wakati wa mchakato wa kuchambua, kuangalia na kupima watiania na hata wagombea, ili kuona kama wana uwezo wa kongoza au wametumia nguvu nyingi ya fedha kupitishwa na vyama vyao.

Kabla ya uchukuaji na urudishaji wa fomu kwa wagombea kuanza na pia mjadala wa upitishaji wa majina haujaanza, kuna jambo ambalo mara nyingi huwafanya wapigakura kushindwa kufanya tathmini ya kina, kwa wagombea kama wanafaa au la.

Ushauri wangu ni kwamba tusiendelee kufunika giza uelewa wetu juu ya kumtambua kiongozi mwenye nia ya dhati ya kuongoza watu, kwa kuangalia zawadi anazotoa, bali uwezo wake wa kuongoza.

Tuachane na mazoea na tabia ya kudharau takwa la kisiasa ambalo ni sehemu ya maisha yetu. Tujitokeze kwa wingi wakati wa kampeni na pia wakati wa kupiga kura ili kupata viongozi bora, si bora viongozi.

Asiwapo mtu wa kushawishika kwa vijisenti vinavyotolewa kama ushawishi wa kuwabadilisha uelekeo sahihi, badala yake muwe na msimamo utakaowawezesha kupata viongozi wenye maono.

> **Mpigakura kutoshiriki mchakato wa kumtathmini mgombea au kushindwa kupigakura siku ya uchaguzi, kunakosesha upatikanaji wa viongozi bora ambao wangesaidia kuleta maendeleo.**

Ikumbukwe kuwa, maendeleo yetu yataanzia pale tutakapokuwa na shauku ya kuchagua viongozi bora wanaotokana na uwezo wao wa kuongoza, si wale wanaotoa chochote, ili wapate uongozi.

Kitendo cha baadhi ya watu kutoshiriki michakato yote hii, kinaweza kusababisha kupatikana na viongozi wasio na sifa za kuongoza. Hivyo kila mwenye sifa za kuchagua, ashiriki kilamilifu.

Mpigakura kutoshiriki mchakato wa kumtathmini mgombea au kushindwa kupigakura siku ya uchaguzi, kunakosesha upatikanaji wa viongozi bora ambao wangesaidia kuleta maendeleo.

Sote tushiriki na kufanya, kuwafanyia tathmini wagombea, ili kupata wale ambao ni sahihi, sio kujiweka pembeni na kukosesha upatikanaji wa viongozi bora wenye maono.

Viongozi bora ni wale wasiotokana na rushwa au ushawishi usio na maslahi mapana ya mitaa. Hivyo, wapigakura wote wajiandae kushiriki katika uchaguzi, lakini wakiwa makini, ili kupata viongozi bora.

Kila Mtanzania ajisikie kuwa maendeleo ya miradi katika kitongoji, kijiji au mtaa wake, yanaendelezwa na yeye kupitia kiongozi atakayemchagua kumwakilisha katika ngazi za maamuzi. Iwapo wananchi wanataka kuondoa vikwazo vya maendeleo kwenye maeneo yao, watambue kuwa kushiriki katika uchaguzi ni muhimu, lakini pia kufanya tathmini kabla ya kuchagua, ni jambo lingine muhimu.

Elimu ya uraia imetolewa ya jinsi ya kuchambua wagombea na hatimaye kupata walio bora, hivyo, elimu hiyo ianze kutumika kuanzia kwenye mchakato wa kura za maoni ndani ya vyama na hata nje ya vyama.

MAKALA

FIKRA MBADALA

# Sera ya CSR si fadhila wala hisani



Pascal Mayalla

SERIKALI kupitia mamlaka za serikali za mitaa, kwa maana ya halmashauri, imekuwa ikitenga asilimia 10 ya mapato ya ndani, kwa ajili ya kutoa mikopo kwa makundi maalumu ya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Mikopo hiyo hutolewa kwa makundi hayo kupitia vikundi vilivyoundwa, kwa ajili ya kuwawezesha kufanya uwekezaji katika miradi midogo midogo, ili kujikwamua kiuchumi. Wanufaika wa mikopo hiyo hawatozwi riba bali wanatakiwa kuirejesha kwa muda uliowekwa, ili kuwe na mzunguko na wengine wanufaike.

Aidha, katika maeneo ambayo wawekezaji wanafanya shughuli zao, hutakiwa kurudisha kwa jamii sehemu ya faida wanayopata. Kama ni wachimbaji wa madini, mafuta, kampuni za biashara mbalimbali na viwanda vya kuchakata mazao, wanapaswa kurejesha kiasi cha fedha kinachotokana na faida, kwa jamii inayozunguka uwekezaji huo.

Fedha hizo si lazima ziwe taslimu, bali zinaweza kuonekana kupitia miradi ambayo inasaidia kutatua kero za wananchi walioko katika maeneo husika. Kwa mfano, wawekezaji hao wanaweza kujenga vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, kutoa madawati, kujenga nyumba za walimu na kuchimba visima vya maji.

Pamoja na kuwapo kwa sera hiyo, baadhi ya kampuni zimekuwa hazitekelezi. Kwa hiyo kama serikali inavyofanya kwa kutoa mikopo, kampuni na taasisi kama vile benki, kupitia sera zao za kurejesha kwa jamii (Corporate Social Responsibility- CSR) zitekeleze na zisione ni hisani au huruma bali ni wajibu.

Mikopo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu, imepachikwa jina la 'Mikopo ya Mama Samia' na ina lengo la kuwajengea uwezo kwa kuwapatia mikopo ya mitaji. Sera za CSR za kampuni na taasisi kurejesha kwa jamii si hisani, inapaswa itungiwe mwongozo, ili isiendelee kuwa hisani wala huruma bali ni wajibu.

Hivi karibnuni kwenye maonesho ya rasilimali za madini mkoani Geita, Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGM), ulichangia Sh. milioni 200 kufanikisha maonesho hayo. Ukiangalia fedha hizo zimefanyia nini, unaweza usiamini.

Sehemu kubwa zimetumika kwa posho, kugharimia vyakula, vinywaji na vitafunwa. Kwa maneno mengine, zimeishia 'Tumbo Street'. Hebu jiulize, fedha hizo kama zinetumika kununua madawati au vitanda hospitalini, wapi ingekuwa na faida zaidi?

Juzi nilihudhuria tukio la utoaji tuzo kwa washindi wa shindano la VIA Creative International Tanzania. Si tu kwamba nimeguswa na kilichofanyika, bali ningetamani kama kampuni zote zinazofanya biashara Tanzania, zitarudisha kwa jamii kitu cha kuonekana na cha kudumu ambacho kitaacha alama.

Katika tuzo hizo, kampuni ya TotalEnergies Marketing Tanzania kupitia sera ya CSR, ilifanya kitu kilichoacha alama. Jambo lililofanyika ni kwenda kwa jamii na kuuliza changamoto zao na kuzipatia ufumbuzi.

Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli, maarufu kama JPM (Mungu amrehemu), aliwahi kufuta hafla ya mchapalo wa Bunge jipya na kuelekeza fedha zinunue vitanda hospitalini. Akafuta gwaride la Uhuru, fedha zikakarabati barabara ya Morocco - Mwenge.

TotalEnergy Tanzania, imeandaa shindano na shule iliyoshinda, Ubungo Makuburi, itapatiwa si tu zawadi, bali changamoto kuu ya shule yao itajibiwa kwa kujengewa ukuta kuizunguka shule hiyo.

Shindano hilo la kimataifa la 'VIA CREATIVE' linanalenga wanafunzi wa shule za msingi wa miaka minne hadi 19, kwa lengo la kuwapatia elimu ya usalama barabarani kwa njia ya sanaa ya michoro, muziki, maigizo na mashairi kisha kuwapa fursa kuelezea uelewa wao na mapendekezo yao ya usalama barabarani, kwa njia ya michoro na maigizo.

VIA Creative ni mradi ulioanza mwaka 2022 ambao tangu mwaka huo, zaidi ya wanafunzi 22,000 wamefikiwa na kujenga klabu za mabolozi wa usalama barabarani kwenye shule 100 Dar es Salaam na Bagamoyo. Mwaka huu mradi huu umewafikia wanafunzi 6,000 kutoka shule za msingi za Makuburi, Ubungo NHC, Buza, Jangwani, Ugindoni na Uzuri mkoani Dar es Salaam na kuendeleza uundaji wa klabu za mabalozi wa usalama barabarani.

Hafla ya kukabidhi tuzo kwa wanafunzi walioshinda kwenye msimu huu wa tatu, ilifanyika kwenye ofisi za kampuni hiyo. Shule ya msingi Makuburi ilibuka mshindi wa kitaifa na mwakilishi wa Tanzania, kwenye ngazi ya kimataifa Novemba, mwaka huu. Shule hiyo pia itazawadiwa kwa kutimiziwa mapendekezo ambayo wanafunzi waliyaomba, kwa ajili ya kuboresha usalama wao barabarani kupitia programu ya VIA Creative.

Mgeni rasmi, Mkuu wa Idara ya Mafunzo ya Kikosi cha usalama Barabarani Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni, Mrakibu Msaidizi (ASP), Rose Maira, alipongeza TotalEnergies, TotalEnergies Foundation na Nafasi Art Space kwa juhudi na mafanikio yao katika kutoa elimu ya usalama barabarani. Alisema juhudi hizo zinapaswa kupongezwa na kuigwa na kampuni zingine, ili kuchochea usalama wa watoto waendapo na watokapo shuleni.

Pia alionyesha furaha baada ya kujua kwamba mradi huo pia una lengo la kutimiza mapendekezo ya kuboresha hali ya usalama kwa wanafunzi wa shule iliyoshinda, kama ilivyooneshwa kuona kwenye filamu ya wanafunzi hao.

Ni wakati sasa wa kuamka na kutoka usingizini kwa serikali kuweka mwongozo na ufuatiliaji kuhusu taasisi kutekeleza sera zao za CSR. Iwekwe bayana kwamba CSR si fadhila, huruma wala hisani bali ni wajibu wa kampuni na taasisi kutoa sehemu ya faida zinazopata na kurejesha kwa jamii.

**Mungu Ibariki Tanzania**
**Paskali**
**Mob. +255 754 270403**

# Katibu wa Bunge aeleza watumishi anachotamani

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraka Leonard, amewataka watumishi wa Ofisi ya Bunge kuendelea kufanya kazi kwa weledi na kwa kujituma, huku wakizingatia kanuni na sheria za kazi.

Leonard aliyassema hayo jana wakati alipokutana na watumishi wa Ofisi ya Bunge, kilichofanyika kwenye ukumbi wa Pius Msekwa.

Alikutana na watumishi hao ikiwa mara ya kwanza tangu alipoteuliwa kushika wadhifa huo na kusisitiza kwamba, watumishi wanafanya kazi kwa kujituma jambo ambalo pia yeye amelishuhudia.

"Nimeelezwa kwamba mnafanya kazi kwa kujituma na mimi nimeshuhudia hilo. Hongereni kwa hilo na naomba mwendelee na ari hiyo ya kufanya kazi kwa kujituma," alisema.

Aliwaeleza pia watumishi hao matarajio yake kuwa waendelee kufanya kazi kwa ushirikiano, nidhamu, upendo na weledi wa hali ya juu.

"Kikao hiki ni muhimu kwangu, ili kuwaeleza yale ninayotarajia kutoka kwenu na mimi niwaeleze ahadi zangu kwenu," alisema.

Katibu wa Bunge aliwakumbusha watumishi hao pia kwamba ushirikiano hauwezi kuwapo sehemu yenye majungu, fitina na ushirikina.

"Naamini katika kufanya kazi kwa ushirikiano. Nafananisha utendaji kazi na timu kama ya mpira, ushrikiano ndio hatimaye unaleta ushindi na watu wanashangilia. Ushirikiano hauwezi kujengwa sehemu yenye majungu. Taasisi yenye amani na upendo kazi inaenda vizuri," alisema.

Pia aliwaeleza watumishi hao kwamba hatawaendekeza wala kuwawavumilia wale wote watakaokuwa wanafanya kazi kwa fitina, majungu, upendeleo na kusababisha migawanyiko.

"Mfanye kazi kwa upendo na palipo na upendo hakuna fitina wala majungu. Sitaweza kuelewana na mtu anayependelea na anayegawanya watu," alisema.

Katibu wa Bunge aliwaeleza watumishi hao kwamba yeye ni mtu anayefikika na siku zote milango yake itakuwa wazi, kwa ajili ya kuzungumza na watumishi au mtumishi yeyote pataka-

# Serikali kuimarisha miundombinu kuwafikia watumiaji gesi kupikia

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dk. James Mataragio, amesema serikali inaendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji na miundombinu ya sekta ya mishati, ili kuwezesha wananchi kufikiwa na huduma stahiki bila kujali umbali na vipato vyao.

Dk. Mataragio aliyasema hayo jana, jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya utoaji Tuzo kwa Mawakala na Wadau wa Kampuni ya Puma Energy Tanzania ambayo inaunga mkono juhudi za serikali za kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia kupitia bidhaa za Puma Gas.

Alisema moja ya majukumu ya Wizara ya Nishati ni kukutana na wadau mbalimbali wakiwamo watoa huduma na watumiaji, ili kuimarisha ushirikiano kati ya sekta binafsi na serikali utakaowezesha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Dk. Mataragio alipongeza Puma kwa jitihada zinazounga mkono juhudi zinazofanywa na serikali katika kuhamasisha jamii kutumia nishati safi ya kupikia, hivyo kutimiza lengo la asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati hiyo ifikapo mwaka 2034.

Alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amekuwa Balozi na kinara katika kuhamasisha matumizi ya nshati Safi ya Kupikia nchini na duniani, ili kuhakikisha watu wanaondokana na matumizi ya kuni na mkaa ambao una madhara kwa afya na kusababisha uharibifu wa mazingira.

Kuhusu tuzo zilizotolewa na Puma Energy Tanzania kwa mawakala na wadau mbalimbali nchini, Dk. Mataragio alielekeza ziwe chachu ya kuendelea kufanya kazi kwa weledi na ufanisi kulingana na vigezo na masharti ya kampuni kwa maslahi ya jamii.

**Alisema kupitia mfano uliooneshwa na Puma Energy Tanzania wa kuwakutanisha wadau wake kila mwaka, ili kuzungumzia mafanikio na changamoto zilizopatikana, iwe chachu kwa kampuni zingine kuiga mfano huo ambao unasaidia kukuza sekta ya nishati nchini.**

Alisema kupitia mfano uliooneshwa na Puma Energy Tanzania wa kuwakutanisha wadau wake kila mwaka, ili kuzungumzia mafanikio na changamoto zilizopatikana, iwe chachu kwa kampuni zingine kuiga mfano huo ambao unasaidia kukuza sekta ya nishati nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa ya Puma Energy Tanzania, Fatma Abdallah, aliishukuru serikali kwa hatua mbalimbali za kuhamasisha matumizi a nishati safi ya kupikia na kuahidi kuendelea kuunga mkono juhudi hizo.

Alisema kampuni yake itaunga mkono kwa kuwafikishia wananchi bidhaa ya Puma Gas, kupitia mawakala na wadau walioko maeneo mbalimbali.

Hafla hiyo pia ilihudhuriwa na Kamishna wa Petroli na Gesi Wizara ya Nishati, Goodluck Shirima.

# HABARI KATIKA PICHA




Mkurugenzi wa Kampuni ya Betty World, Jesse Madauda (wa pili kushoto) na Mshauri wa Magonjwa ya Ngozi kutoka nchini Kenya, Cyndy Muriro (kulia), wakikata utepe, kuzindua mafuta ya ngozi yaliyotengenezwa mahususi kwa watu wenye ngozi nyeusi, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Kushoto ni Mbunifu wa bidhaa hiyo hapa nchini, Dk. Elizabeth Consoli na Mtaalam wa Magonjwa na Afya ya Akili Kimataifa, Michelle Chapa (wa pili kulia). **PICHA: JUMANNE JUMA**



Wafanyabiashara wadogo wakiwa wamepanga bidhaa zao chini wakisubiri wateja katika eneo la Kariakoo jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Irene Gowelle, akitoa maelezo kwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Zanzibar, Dk. Shaibu Hamis Kaduara (wa pili kulia), wakati alipotembelea banda la shirika hilo katika Kongamano la 10 la Jotoardhi Barani Afrika, lililofanyika jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Baadhi ya washiriki wa Kongamano la 10 la Jotoardhi Barani Afrika, wakifuatilia hotuba ya Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Dk. Shaibu Hamis Kaduara, lililofanyika jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa barabara ya mabasi ya mwendokasi katika eneo la Tegeta, Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MAISHA

Oktoba 27, 2024
Nipashe


Baba, Mam ... ili




# Namna ya kutunza ngozi ya miguu

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| U | | C | H | A | M | A |
| T | | | | N | | N |
| A | | Z | N | Z | | Z |
| W | A | O | | I | P | I |
| A | | N | O | A | | S |
| L | | G | | | | H |
| A | M | A | N | I | | A |

## AMSHA AKILI


MSAIDIE PAKA APATE NJIA YA KWENDA KUMKAMATA PANYA



## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

BAA, SAA, RAI, KOO, UKAME, MAMBO, BISHA, MWAKA, ONGOPEA, AJARIBU

## WATOTO

# PAKA RANGI







Alichokifanya daktari

Mama mmoja alikuwa anafanya usafi chumbani na ghafla aliona kisanduku chini ya uvungu wa kitanda cha mtoto wake.

Alipokifungua akakuta mawe madogo 15 yakiwa ndani, ndipo alipokwenda kumuuliza mtoto ake.

Mama: Kisanduku hiki cha nini?

Mtoto: Mama kisanduku kina mawe yangu

Mama: Ndiyo, haya mawe ya nini?

Mtoto: Mama nisamehe, hayo mae nilikuwa nayaweka kila nikiiba yai la kuku wako.

Mama: Wee mtoto yani umeshakula mayai 15, sasa nitakuadhibu

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Laana ilivyo chanzo cha matatizo mengi

KARIBU tena msomaji wangu kwenye safu yetu. Maisha ni fumbo lililobeba mambo mengi sana. Leo hebu tuangalie kidogo maana ya laana na jinsi inavyotesa watu wengi.

Laana ni maneno yenye nguvu inayoharibu maisha ya mtu pale yanapotamkwa. Ni kukosa rehema za Mungu. Ni kitu kinachokukamata, ili usipige hatua.

Aidha, laana ni ukosefu wa radhi za Mungu katika jambo fulani. Radhi ni msamaha, kwa hiyo, laana ni ukosefu wa msamaha wa Mungu katika jambo fulani.

Kuna laana pande mbili, laana iliyo wazi inayoonekana na ile iliyojificha ambayo tunatembea nayo, lakini hatuioni. Yaani hatujui ni kwa nini mambo fulani yanatupata tukidhani ni kawaida tu.

Kuna laana hutolewa na wanadamu kama maapizo na hizi zimewakamata watu wengi, kwa sababu hawaombi na wala hawajui haki zao kwa Mungu. Wameteswa sana na laana hizo, huku wakijifariji kwamba wamekombolewa kutoka laana kama baadhi ya maandiko ya Mungu yanavyoainisha.

Yako mambo umeyaona kwenye ndoto au maono yakionyesha wachawi au wakuu wa giza wakikulaani. Kumbe unapaswa kuomba na kufuta, vinginevyo laana hiyo hakika itakupata, huku ukibaki kujifariji kwamba umekombolewa kutoka laana.

Nimetaja hapo juu kwamba kuna laana iliyo wazi na iliyojificha, hatuioni na hatujui ni kwa nini tupo vile tulivyo. Ni sawa na kimbunga au upepo mkali ambao hujui utokapo wala wapi unakoelekea.

Unaweza kwenda sehemu ukapaona ni pazuri kwa mwonekano, lakini wakazi wake hawana maendeleo. Hakuna nyumba mpya ni za ovyo ovyo, watu wake hawana mwamko wa kimaendeleo.

Ukionekana unainuka unapigwa vita. Kumbe yako maneno ya laana yalishatamkwa kwamba hakuna kuzidiana, lazima wafanane fanane tu.

Lakini pia kuna laana imejificha ambayo itatenda kazi kwa majira na nyakati fulani. Kwa mfano, inakusubiri upate fedha ndipo ionekane, unapata fedha majanga yanaibuka kwenye familia.

Mtu anapokutamkia kwamba “na tuone kama utafanikiwa”. Haya ni maneno mazito sana na usipokuwa makini ukamuomba Mungu na kuyafuta, kweli hutafanikiwa.

Wako watu wengi wanateseka leo kisa ni maneno waliyotamkiwa ama na wazazi wao, majirani, marafiki au mababu na mabibi zao katika nyakati tofauti.

Yuko jirani mtagombana akatamka maneno kwamba binti yako au kijana wako hataolewa au hataoa. Na maneno haya yakatokea kama yalivyotamkwa. Hiyo ni laana usipoishughulikia kwa maombi na kuifuta itakutesa.

Msomaji wangu, hebu sasa tuangalie baadhi ya vyanzo vya laana. Kwanza ni dhambi. Ukitenda dhambi unaweza kulaaniwa. Mtu alipozini tu akalaaniwa. Kuna laana inasababisha mnyororo wa matukio katika familia.

Chanzo kingine ni kurithi. Yako matatizo unayo kumbe yalisababishwa na wazazi wako. Neno la Mungu linasema, “Baba zetu walitenda dhambi hata hawako; Nasi tumeyachukua maovu yao” (Maombolezo 5:7).

Chanzo kingine ni wachawi. Mtu anakwendea kwa mganga wa kienyeji ambako yule anayelogwa anatamkiwa maneno mabaya. Mfano mganga anaambiwa mfunge fulani kizazi, ili asizae.

Wako wakinamama wengi wanapoteza maisha kabla au wakati wa kujifungua, kumbe yapo maneno yaliyotamkwa na mchawi kwamba hatapata watoto/wajukuu atakufa.

Kwa mfano, yuko dada mmoja alikuwa akitoa ushuhuda kanisani akasema, kwao wapo ndugu watano na hadi sasa hawajaolewa wala hakuna hata mmoja aliyebahatika kupata mtoto.

Kumbe yuko shangazi yao mshirikina aliwahi kutamka kwamba watoto wa kaka yake hawatakaa waolewe na ikawa hivyo. Hakika, hakuna jambo linalotokea kwa bahati mbaya pasipo kuwa na chanzo!

Hivyo, kutamkiwa maneno mabaya ni chanzo cha laana. Usipoyafuta kwa maombi maneno hayo yamebeba nguvu nyuma yake, yatakayosababisha matokeo mabaya katika maisha ya mtu. Usipuuzie maneno yanayotamkwa!

Kushika vitu vilivyolaaniwa pia ni chanzo kingine cha laana. Pia kuishi au kulima katika ardhi iliyodhulumiwa nawe utalaaniwa.

Chanzo kingine cha laana ni mawakala wa shetani, pesa za dhuluma, kuzaliwa kwenye madhabahu za shetani (watoto wanaopatikana kupitia kwa waganga). Kupeleka pesa kwa mganga na hata ‘kushea’ kitanda na mganga.

Sasa utamjuaje aliyelaaniwa? Maandiko ya Mungu yanasema kwamba utalaaniwa mjini, utalaaniwa na mashambani. Utalaaniwa uzao wa tumbo lako.

***Mazuri yanageuka mabaya, utashindwa na maadui zako, utaonewa, utakusanya wengine watakula na utafanya kazi sana faida kidogo! Je, una maoni? Ujumbe 0715268581. Namba ipo pia WhatsApp.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Ajali mtaka vitu zinavyohusishwa na kazi ya Mungu

NDANI ya wiki moja, tumewapoteza Watanzania wenzetu 19 kutokana na ajali za barabarani. Ajali za barabarani sasa ni tishio la uhai wa binadamu. Kila kona ni vilio, simanzi na huzuni.

Madereva wanapuuza sheria za barabarani, wanalewa na hakuna hatua za kuwapima zinazochukuliwa. Nchi imepoa!

Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), mmejisahau na huo ndio ukweli. Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, punguzeni ushikaji na madereva, makondakta.

Nawaza tu, tuna LATRA CCC? Kama wapo kwa nini haya yanatokea mfululizo? Mara ya mwisho ni lini mmetoa elimu kwa Watanzania kuhusu tahadhari ambayo abiria wanaweza kuchukua kujinasua na bundi wa ajali za barabarani?

Nilitarajia au Watanzania wanatarajia kuona LATRA, LATRA CCC na Polisi wanafanya elimu na uhamasishaji. Kwamba mnaimarisha kampeni za elimu kuhusu usalama barabarani kwa madereva na watembea kwa miguu. Uko wapi ule ukaguzi wa mara kwa mara wa magari barabarani unaofanywa na wakaguzi wa vyombo vya moto?

Namaanisha ule udhibiti na kuweka masharti madhubuti wa ukaguzi wa magari, ili kuhakikisha yanatumika tu pale yanapokuwa katika hali nzuri. Sioni uimarushaji wa sheria, tunaweka sheria kali dhidi ya uendeshaji wa hatari kama kuyapita magari mengine bila kujiridhisha na hatari iliyoko mbele yake, kulewa na kuendesha bila kuwa na leseni iliyohakikiwa.

Wakala wa Barabara Tanzania TANROADS, mnafanya kazi nzuri sana, lakini fanyeni maboresho ya miundombinu kwa sababu mingi ni chanzo cha ajali. Mfano ufinyu wa daraja la Kikavu katika barabara kuu ya Arusha-Moshi, linapitika kwa tabu kutokana na ongezeko la malori ya nchi jirani yanayokwenda Kenya na Bandari ya Tanga.

Serikali yangu tukufu. Fikirieni upya na mje na mpango mkakati wa mifumo ya usalama. Litakuwa jambo zuri sana kama tutaweka mifumo ya kamera za ufuatiliaji barabarani na teknolojia nyingine za usalama.

Jambo jingine, ifike mahali jamii na madereva tujenge utamaduni wa usalama. Watanzania hatuna utamaduni mzuri wa usalama kwa jamii, ikiwa ni pamoja na kutoa motisha kwa madereva wenye rekodi nzuri. Kama tutafanya mabadiliko haya, kuna uwezekano wa kupunguza ajali za barabarani.

Nayasema haya kwa makusudi kwa sababu mwanzoni mwa wiki hii, tuliwapoteza waimbaji watano ambao ni wanakwaya ya Usharika wa Wazo Hill wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

Mbali na waliopoteza maisha, wenzao 20 walijeruhiwa katika ajali ya basi iliyotokea eneo la Kirinjiko Airtel, Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro. Wanakwaya waliopoteza maisha ajalini, walikuwa wakitokea jijini Dar es Salaam kuelekea Machame, Wilaya ya Hai, kwenda kushiriki maziko ya mwanakwaya mwenzao aliyefariki dunia, wakati akijifungua.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Kasilda Mgeni, amenukuliwa akisema waimbaji hao wa Usharika wa Wazo Hill, walipata ajali hiyo alfajiri ya Oktoba 22 mwaka huu, baada ya basi dogo aina ya Toyota Coaster (Special Hire), kuacha njia na kugonga kalavati.

Basi hilo lilikuwa likiongozana na mabasi mengine manne ya aina hiyo na dereva wake inaelezwa alisinzia na ghafla na aliposhtuka alibaini tayari ameshaligonga.

Katika ajali hiyo waliofariki dunia na kutambuliwa, ni watu watatu ambao ni Stephen Temba (40), Aurelia Swai (50), Neema Ngusi (35), Charles Mchome (63) na Maderina Mtenzi (58).

Kutokana na ajali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, aliwataka madereva kuchukua taadhari nyakati zote, huku akiwataka kukumbuka wamebeba maisha ya watu.

Tunatoa pole sana kwa familia, ndugu jamaa na marafiki ila nimepata taarifa wanaendelea na matibabu na baadhi wamekimbizwa hospitali za rufani zilizopo mkoa wa Kilimanjaro kwa matibabu zaidi,” alisema mkuu huyo.

Kimsingi, hii ni ajali ya pili mkoani Kilimanjaro kutokea katika muda usiozidi siku saba, Oktoba 19 mwaka huu, watu wengine 14 walifariki dunia na wengine 12 kujeruhiwa vibaya kwenye ajali, iliyohusisha magari matatu, basi dogo Toyota Coaster, Toyota Hilux na lori la mizigo aina ya Scania.

Ajali hiyo iliyotokea katika daraja la Mto Kikavu, Wilaya ya Hai, ilihusisha lori la mizigo aina ya FAW, lenye namba T 517 EAE lililokuwa na Tela namba T 287 CYF,

liligonga kwa nyuma gari namba T 553 aina ya Toyota Hilux (Pick up), ambalo lilipoteza mwelekeo na kwenda kugongana uso kwa uso na basi dogo aina ya Toyota Coaster namba T 525 DKP.

Ajali hizo zimemsononesha Rais Samia na katika mtandao wake wa kijamii wa WhatsApp channel, ameandika: “Nimepokea kwa masikitiko taarifa za ajali za barabarani zilizotokea katika mikoa ya Mwanza na Kilimanjaro na kusababisha vifo na majeruhi. Nawapa pole wafiwa wote, familia, ndugu, jamaa na marafiki. Nawaombea marehemu wapumzike kwa amani, na majeruhi wote wapone kwa haraka.

“Tunapoelekea mwishoni mwa mwaka, nawasihi watumiaji wote wa barabara kuongeza umakini. Nimeziagiza mamlaka zote husika kuongeza umakini katika usimamizi wa sheria za usalama barabarani.”

Mwenyezi Mungu azilaze roho za ndugu zetu hawa mahali pema peponi. ‘


***• Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***











Ilikuwa siku ya furaha kwa Dainess Kitanzimwa na Hamisi, kufunga ndoa takatifu katika Kanisa Katoliki Kamelaiti, Morogoro na sherehe ya kuwapongeza ilifanyika katika ukumbi wa Mambo Club mkoani humo.

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo

## Tamba na fulana za mistari







FULANA maalum ya mistari yenye shingo ya mitindo tofauti, inaleta ladha ya kipekee katika mwonekano wa kila mtu.

Muundo wa nguo hii inampa mvaaji starehe na furaha muda wote kutokana na kuupa mwili uhuru zaidi.

Kitambaa cha unyevu na mtindo tofauti huhakikisha mwili kupumua kwa kiwango cha juu na uhemaji ulio sawa.

Wanaopenda kuvaa aina hii ya nguo ni lazima kutambua kwamba chaguo zuri la michoro, rangi na muundo wake ndio inakupa matokeo mazuri.

Kwa wale wanaopenda kuongeza nakshi zaidi, unaweza kuchapisha picha, nembo au namba mbele au nyuma.

Fulana hizi zimeundwa kutokana na vitambaa laini, vyepesi, kwa ajili ya kumudu harakati zako ikiwamo mazoezi.

Mikono mifupi hutoa nafasi ya kufanya kila unachotaka pamoja na kuweka hata mikono yako.

Changanya na nguo zingine, ili kuleta msisimko zaidi kama vile suruali ya kitambaa, jeans, kaptula ya aina yoyote na hata suruali ya mazoezi.


Chini una chaguo pana kwani kila aina ya viatu unaweza kuvaa na ukatoka bomba zaidi.

**PICHA ZOTE: PINTEREST**

URJEMBO

Na Mary Geofrey

# Namna ya kutunza ngozi ya miguu



JE, unajua ngozi ya miguu inatoa nafasi ya watu kuonekana watanashati zaidi? Basi kutokana na umuhimu wake, leo tunajifunza utunzaji wa ngozi ya muguu kwa kutumia bidhaa zinazopatikana jikoni kwako.

Miguu ni kiungo kinachofanya kazi kila wakati, kutembea hapa na pale. Kinapigwa vumbi, jua na hata baridi.

Hivyo usipo itunza inakuwa mikavu, migumu na yenye mipasuko. Matunzo ya miguu, fanya kama mara mbili kwa wiki.

Pasha maji moto hadi yawe ya uvuguvugu lita tatu, halafu yaweke kwenye beseni.

Kamulia ndimu kwenye maji, weka na chumvi ya mawe kijiko kikubwa kimoja. Changanya vizuri, kisha weka miguu yako kwenye beseni, hakikisha miguu (feet) imezama vizuri kwenye maji na iloweke kwa dakika 15 hadi 20.

Kuloweka miguu kwenye maji ya chumvi na ndimu, inasaidia ngozi ya nyayo za miguu kulainika haraka, hivyo ukija kusugua gaga au 'dead skins' inatoka kwa urahisi.

Pia kuondoa harufu kwenye miguu na vilevile kutengeneza mazingira yasiyo rafiki kwa bakteria kuishi kwenye miguu yako.

Baada ya kuloweka miguu, kifuatacho ni kusugua gaga, hapa kazi inakuwa rahisi sana, sababu nyayo zinakuwa ziko laini.

Tumia jiwe laini kusugua gaga, unasugua taratibu hadi uone ngozi zilizokufa zimetoka zote.

Kisha kung'uta miguu vizuri, inawishe na maji halafu ikaushe vizuri kabisa.

Baada ya hapo paka mafuta, 'lotion' au 'cream' kutegemea na wewe unachotumia.

Ukimaliza kaa pumzika iache miguu ipate hewa kabla ya kuendelea na mambo mengine

Kama una fangasi miguuni hakikisha umepata dawa kutoka kwa daktari utumie hadi upone, ndio uje kuendelea na mambo haya.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Mihogo ya kukaanga



KATIKA msimu wa mihogo ni muhimu ukafurahia chakula hiki nyumbani kwako na sio mitaani kama ilivyo kawaida ya wengi.

**Mahitaji**

Mihogo mikubwa mitatu, mafuta lita moja, kitunguu kimoja, kitunguu saumu kiasi, tangawizi kiasi, nyanya nne, limao moja, karoti nusu, hoho nusu, chumvi na pilipili.

**Namna ya kupika**

Menya mihogo, ikatekate kiasi upendacho na kwa urahisi wa kuiva kisha ikoshe bandika karai, tia mafuta, yakipata moto weka mihogo ukaange, angalia moto usiwe mkali sana, ili mihogo iive polepole bila kubabuka.

Ikiishaiva itoe na iweke kwenye chujio, ili kuondoa mafuta vizuri. Anza kuandaa kachumbari yakulia mihogo.

Osha nyanya, karoti, hoho, tangawizi, chukua sufuria uvisage uvitie, kisha katakata kitunguu tia, twanga pilipili uitie pia.

Weka chumvi na pilipili manga na bandika jikoni uweke na maji nusu kikombe na unyunyuzie mafuta kiasi. Funika acha ichemke kiasi dakika tano.

Kisha tia limao uache ichemke kidogo, epua kachumbari yetu yakulia mihogo tayari.

Sasa mihogo yetu tunaweza kuila muda wowote, kwa chai, maji na hata juisi na hata ukipata samaki wakukaanga hunoga zaidi. Na si lazima uwe na kachumbari waweza kula na tomato, chili si mbaya,

## Pamba chumba cha kulala



**Na Restuta James**

NI Jumapili nyingine ambayo Nipashe inakuletea maarifa ya namna ya kuifurahia nyumba yako.

Chumba cha kulala ni eneo muhimu linalohitaji kumtuliza mtu na kazi za kutwa, hivyo ni busara kutengeneza mazingira ya kuhakikisha unapata pumziko zuri wakati wa usiku.

**KITANDA, MASHUKA NA MITO**

Kimsingi hivi ndivyo vinavyofanya chumba kiitwe cha kulala maana ni wazi huwezi kukuta kitanda jikoni. Wataalamu wa mapambo wanashauri kuwa kamwe usikurupuke kitandani ukakiacha kikiwa rafu bila kutandika.

Wanasema kukiacha hivyo kutakupa uvivu wa kukiweka vizuri wakati wa kulala usiku, kwa kuwa unaweza kurudi ukiwa umechoka.

Mito mingi inavutia kitandani hasa kama unalala peke yako. Pia rangi za mashuka ziwe tulivu, lakini zisiwe za giza japokuwa sio lazima ziwe nyeupe.

**ZULIA**

Kama huwezi kununua linalotosha chumba kizima, ni vyema ukaweka dogo, ili unapoamka miguu yako isikanyage moja kwa moja sakafu ya baridi. Pia linasaidia kukupa nafasi ya kuomba ukiwa umepiga magoti, tofauti na sakafu ambayo inakuwa ya baridi.

**TAA YA KIVULI**

Taa hii inatumika kama pambo linaloamua kiasi cha mwanga unachohitaji pale unapohitaji kusoma au kufanya kitu kisichohitaji mwanga mwingi.

**SOFA**

Ni muhimu kuwa na sehemu ya kukaa chumbani, kwa ajili ya mazungumzo au kusoma. Eneo hili linasaidia kuweka matandiko vizuri pindi unapotandika kitanda.

**PICHA, SAA**

Picha ya kuchora inapendeza zaidi chumbani. Inaweza kuwekwa kwenye ukuta unaotazamwa na mtu aliyelala kitandani. Pia ukuta huu unaweza kuwekwa saa, japokuwa wengine hupendelea kuweka saa juu ya droo za pembeni ya kitanda.

**PAZIA**

Chumba cha kulala kinahitaji faragha na hisia za giza hata kama kimenakshiwa kwa rangi za mwanga. Pazia sahihi zitakamilisha faragha.

**Tuwasiliane katika 0753333330.**

**Na Elizabeth Zaya**



# RATIBA YA USAFI WA NYUMBA NI MUHIMU SANA

USAFI wa nyumba ni moja ya mambo muhimu katika ustawi wa maisha ya mwanadamu. Nyumba inapokuwa safi kwa maana ya mazingira na mpangilio, inafanya afya ya watu wanaokaa ndani kuimarika.

Kwa mantiki hiyo, usafi wa nyumba unapaswa kufanyika mara kwa mara ndani na nje, ili kuifanya ivutie na kuwafanya watu wapende kuwapo muda wote. Nyumba inapopendeza ni pambo zuri.

Kinyume cha hapo nyumba inapokuwa chafu, inasababisha pia watu kuwa katika hatari ya kuwa na madhara kiafya. Uchafu unachangia kwa kiwango kikubwa kuharibu nyumba hata kama ni nzuri na iliyojengwa katika uimara kiasi gani.

Mwingine anaweza kusema mbona kusafisha nyumba ni jambo linaloeleweka? Lakini ninachotaka kueleza ni kwa namna gani unatakiwa kuweka kipaumbele na kujiwekea ratiba nzuri ya usafi wa nyumba yako yote.

Kumbuka kwamba nyumba ikisafishwa kwa umakini na ufasaha ni dawa inayojitosheleza katika kuimarisha na ikadumu zaidi kama ambavyo ni kinyume kama isiposafishwa vizuri, ina uwezekano mkubwa wa kuharibika na kupoteza mvuto na uimara wake.

Jambo la msingi na la kuzingatia ni kwamba nyumba ina maeneo mengi na kila eneo linahitaji kusafishwa kwa umakini, kwa ajili ya ustawi wake.

Ili ufanikiwe katika hilo ni lazima kujiwekea utaratibu mzuri wa kujipangia ratiba ya namna gani bora ya kufanya usafi katika kila eneo la nyumba yako.


Kwa mfano kama ni jikoni, chumbani, sebuleni, jikoni, nje ya nyumba, stoo, vyooni na katika viunga vyote vya nyumba, hakikisha kwamba kote kunafanyiwa usafi wa uhakika kila mara.

Kwenye maeneo yote ya wazi yakiwamo yale yanayohitaji kufagiliwa, hakikisha unafanya hivyo. Kama umepanda maua, yahudumie nayo vizuri kwa kuyawekea mbolea na kuyamwagia maji pamoja na kuyatengenezea mazingira ya kuendelea kustawi zaidi na yasigeuke kuwa uchafu kwenye nyumba.

Baada ya kufanya usafi hakikisha unakagua kila eneo la nyumba, ili kujiridhisha kama endapo kila mahali kumeguswa na usafi na kama kuna vitu ambavyo havihitajiki au havitumiki, viondoe.

Pia baada ya kusafisha hakikisha kila kitu kwenye nyumba kimepangiliwa inavyostahili kuanzia jikoni, sebuleni, vyumba vya kulala, vyooni na hata nje ya nyumba kwenye bustani na sehemu nyinginezo.

Hakikisha yale maeneo yote ambayo yanahitaji kufanyiwa usafi kila siku inafanyika hivyo na kwenye kila eneo la nyumba yako, ndio utaiimarisha lakini endapo hakutakuwa na mpango mzuri wa kuisafisha, utaiharibu.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
HUKU 'SIMBAWANGA' UKIJA MPYA LAZIMA SISI WAKULUNGWA TUKUKARIBISHE KWA STAILI MAALUMU
WOOOOYEEEEEE!!! NIMELIFYEKA JITU NIMELIKAANGA ROHO MCHANA KWEUPEEEE MBUZI ANAKULA MAJANI HA HAAAA!
'THIKUBALI' "KALUMANZILA" ANIRUDISHIE HELA ZANGU SIVYO NAENDA JELA
SINA PAPARA WE' BIDUKABIDUKA LAKINI NITAKUTIA MBARONI ITAKUWA ZAMU YANGU
OYA SOJAAAA 'MACHEJO' UNAYEWEZA?
MAPENZI NI KAMALI 'UKIPUNWA' SEPA ZAKO, HIYO SURA YA HURUMA PELEKA KWA MKEO
NAENDA KUSEMA NINI WAKATI KIINUA MGONGO CHANGU 'UMEKIBEMENDA' NIPO MTUPU!
MKE WANGU KANIDUNDA MPAKA ASUBUHI KAMA ANAPIGA NGOMA! HAPA NILIPO NAFICHA SIRI KANIUA KIZAZI
SI AFADHALI YA WEWE! MWENZAKO MAINI YOTE SINA NATEMBEA KWA KUDRA TU!
USINITANIE MIMI NI MKWEO UMENIOLEA BINTI YANGU
UMESAHAU NILIVYOKUFUMA NA DADA'ANGU UKAUTELEKEZA MSULI?
UKISHINDWA KUTOBOA MAISHA, TOBOA PUA

## HABARI KIMATAIFA



Wakazi wa mji wa Tehran, nchini Iran, wakiangalia milipuko ya makombora iliyofanywa na Israel kusini mwa mji huo, jana. **PICHA: REUTERS**

# Watu 300 mbaroni Msumbiji

**MAPUTO,** MSUMBIJI

WATU 300 wamekamatwa na polisi nchini Msumbiji, wakati wa maandamano ya kupinga matokeo.

Maandamano hayo yaliibuka baada ya Tume ya Uchaguzi kutangaza ushindi kwa Daniel Chapo, ambaye ni mgombea wa chama tawala cha FRELIMO katika uchaguzi wenye utata uliofanyika wiki mbili zilizopita.

Kulikuwa na maandamano yaliyoambatana na ghasia katika miji kadhaa nchini humo, juzi usiku, baada ya tangazo hilo.

Hata hivyo, mgombea wa upinzani Venancio Mondlane, ameitisha maandamano hayo akidai kuwapo kwa udanganyifu katika upigaji kura.

Hali ya utulivu ilirejea muda mfupi baada ya maandamano hayo.

Polisi walithibitisha wakamata watu 370 nchini kote wakati wa makabiliano na waandamanaji na watu wanaodaiwa kupora mali.

Hata hivyo, mtu mmoja alithibitishwa kufariki.

**BBC**

# Israel yaishambulia tena Iran

**TEHRAN,** IRAN

ALFAJIRI ya jana, miji kadhaa ya Iran ilishuhudia milipuko ya makombora baada ya Israel kufanya mashambulizi ya anga ya kulipiza kisasi.

Israel imefanya mashambulizi kadhaa ya anga ikilenga kambi za kijeshi na viwanda vya kutengenezea makombora katika miji mitatu.

Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF), lilisema kuwa lilifanya mashambulizi mahususi dhidi ya vituo vya kijeshi nchini Iran, kama njia ya kulipiza kisasi kwa shambulio la Oktoba Mosi, mwaka huu.

Uthibitisho wa IDF wa kuishambulia Iran ulifuatia ripoti za vyombo vya habari vya Iran, kuhusu kusikika kwa milipuko kadhaa ndani na karibu na mji mkuu wa Tehran.

Iran iliishambulia Israel kwa kurusha zaidi ya makombora 200 ya balistiki, kuelekea Israel katika kile ilichosema kulipiza kisasi mauaji ya kiongozi wa kisiasa wa Hamas katika ardhi ya Iran, Julai.

Msemaji wa IDF, Daniel Hagari, alisema Israel ina haki na wajibu wa kujilinda na "uwezo wake wa kujihami na kushambulia.

Marekani, mojawapo ya washirika wa karibu wa Israel, ilisema shambulio la Jumamosi dhidi ya Iran, ni zoezi la kujilinda.

Vikosi vya ulinzi wa anga vya Iran vilisema katika taarifa yake kwamba, kambi katika mikoa ya Tehran, Khuzestan na Ilam, zilishambuliwa.

Hata hivyo, vilieleza mashambulizi hayo yalizuiliwa kwa mafanikio na kusababisha uharibifu mdogo katika baadhi ya maeneo.

Mtaalamu mmoja wa kisiasa alisema, anasema kauli hiyo ni dalili za mapema zinaweza kuashiria kuwa Iran inajaribu kupunguza uwezekano wa kuendelea kwa mzozo huo.

Upande wa jeshi la Israel, lilisema kuwa mashambulizi dhidi ya maeneo yaliyolengwa yamekamilika.

"Muda mfupi uliopita, IDF imekamilisha mashambulio dhidi ya malengo ya kijeshi katika maeneo kadhaa nchini Iran," ilisema taarifa hiyo.

"Ndege zetu zimerejea nyumbani salama." Iliongeza.

Baadae, Hagari alijitokeza na kusema Iran imelipia gharama kwa mashambulizi yake ya hivi karibuni dhidi ya Israel.

Alisema Israel ilifanya mashambulio sahihi na yaliyolenga shabaha katika maeneo tofauti nchini humo.

Malengo hayo yalijumuisha vituo vya kutengeneza makombora, maeneo ya kurusha makombora kutoka ardhini na uwezo mwingine wa angani.

Alieleza kwamba, Israel ilichagua maeneo hayo miongoni mwa mengine yanayolengwa na kuwa huenda ikuchagua shabaha za ziada kuzishambulia ikiwa itahitajika.

"Huu ni ujumbe wazi wale wanaotishia Taifa la Israel watalipa gharama kubwa," aliongeza.

Hata hivyo, Marekani imeitaka Iran kutolipiza kisasi kwa kuishambulia tena Israel.

"Iwapo Iran itaamua kujibu kwa mara nyingine, tutakuwa tayari na hatua hiyo itakuwa na madhara kwa Iran kwa mara nyingine," ilisema taarifa ya maofisa wakuu wa serikali ya Marekani.

Iliongeza kuwa Marekani haitaki kuona hilo likitokea.

"Hii inapaswa kuwa mwisho wa makabiliano haya ya moja kwa moja kati ya Israel na Iran," ilisisitiza taarifa hiyo.

Iliongeza kwamba Marekani iko tayari kuongoza juhudi za kuhitimisha vita vya Lebanon na kujaribu kufikia usitishaji mapigano Ukanda wa Gaza, pamoja na kurudishwa kwa mateka wa Israel.

Siku chache kabla ya shambulizi hilo, Rais Joe Biden alisema Israel ina haki ya kujilinda na kujibu mashambulizi ya Iran.

Hata hivyo, Biden aliiambia Israel kuwa hataunga mkono shambulio lolote linalolenga vituo vya nyuklia vya Iran, kwa kuhofia kwamba linaweza kusababisha kuongezeka kwa mzozo unaozidi kufukuta.

Pia alisisitiza kuwa Marekani haitaunga mkono shambulio la Israel dhidi ya miundombinu ya mafuta ya Iran.

Vyombo vya habari vya serikali ya Iran, vimethibitisha kuwa milipuko imesikika katika eneo la magharibi mwa Tehran. Wizara ya Ulinzi ya Marekani, ilisema kuwa kwamba Marekani ilifahamishwa kuhusu mipango ya Israel kabla ya kutekelezwa kwake, lakini Marekani haikushiriki katika operesheni hiyo.

Hatua ya Marekani kutoshiriki katika mashambulizi hayo hayo ni juhudi za kujaribu kuzuia mzozo kati ya Israel na Iran kuzidi kuongezeka.

Matokeo ya athari iliyotokana na mashambulizi hayo yataonekana baada ya hali kutulia.

Tathimini hiyo inajibu maswali kama Israel, ililenga pekee maeneo ya kijeshi au alivuka mipaka na kujumuisha vituo vya mpango wa nyuklia wa Iran, jambo ambalo linaweza kusababisha ulipaji wa kisasi.

**BBC**

HABARI/SAFU

# Mafanikio mawasiliano TEHAMA yaivuta Mali kujifunza Tanzania

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA




KATIBU Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mohammed Khamis Abdulla) (pichani), amepokea na kuikaribisha timu ya wataalamu kutoka Mali, kwa ajili ya kujifunza kutoka Tanzania namna ya kuratibu na kusimamia masuala yanayogusa sekta za mawasiliano na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Akizungumza na ujumbe huo juzi wizarani Dodoma, Abdulla alisema wizara na taasisi zake ziko tayari kutoa ushirikiano kwa kuwa kuna maeneo mengi ambayo Mali inaweza kujifunza Tanzania yakiwamo masuala ya akili mnemba (AI).

"Kama nchi kupitia wizara hii, tuna mafanikio na mipango mingi ambayo iko kwenye hatua za utekelezaji ikiwamo kujenga chuo kikubwa cha umahiri cha TEHAMA na kituo kikubwa zaidi cha kuhifadhia data, hivyo mnakaribishwa sana kujifunza kutoka kwetu," alisema.

Ibrahima Abdoulaye Kone, kiongozi wa wataalamu hao wa Mali, alisema nchi yake ina mengi ya kujifunza kutoka Tanzania hasa katika muundo wa kitaasisi, umoja na ushirikiano uliopo kwa taasisi zinazoshughulikia masuala ya mawasiliano na TEHAMA.

Alisema nchini Mali, uratibu na usimamizi wa taasisi zinazojihusisha na masuala ya habari, mawasiliano na TEHAMA hauko katika wizara moja kama ilivyo kwa Tanzania, hivyo kusababisha baadhi ya maeneo kushindwa kuratibiwa vyema.

Aliongeza kuwa asilimia 99 ya wananchi wa mali wanamiliki simu janja na bei ya kifurushi cha data kwa GB moja ni sawa ni dola za kimarekani mbili (sawa na Sh. 5,500 za kitanzania).

Wataalamu hao kutoka Mali wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano na Posta ya Mali (AMRTP) na Wakala wa Usimamizi wa Mfuko wa Upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano kwa Wote (AGEFAU), wako nchini kuanzia Oktoba 21 hadi leo, kwa ajili ya kujifunza na kubadilishana uzoefu na wizara, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na kampuni ya simu ya Airtel.

# Wafurahia kupata elimu kuhusu fedha

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

BAADHI ya wakazi wa Jiji la Mbeya, wameipongeza serikali kwa kuwasogezea elimu ya fedha na huduma mbalimbali za kifedha karibu nao.

Wananchi hao walitoa pongezi hizo juzi katika Maadhimisho ya Nne ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa ,yanayoendelea katika viwanja vya Ruanda-Nzovwe, jijini hapo.

Walisema elimu wanayoendelea kuipata katika maadhimisho hayo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi wao binafsi na taifa kwa ujumla.

Rehema Kassiba wa Kumekucha SACCOS, mmoja wa wananchi hao, alisema maadhimisho hayo yamewarahisishia upatikanaji wa elimu na huduma za fedha kwa kuwa serikali imesogeza huduma muhimu za masuala ya kifedha katika maadhimisho hayo.

Aliipongeza serikali kwa kuandaa maadhimisho hayo na kuahidi atakuwa balozi mzuri kwa kuifikisha elimu aliyoipata kwa wananchi wengine ambao hawajapata nafasi ya kufika viwanja vya Nzovwe yanapofanyika maadhimisho hayo.

"Elimu hii ni nzuri na muhimu kwetu lakini tunaiomba serikali iandae utaratibu wa kufikisha elimu hii katika maeneo ya vijijini kwa kuwa muda wa maadhimisho haya ni mfupi, hivyo si rahisi kwa wananchi wote kuhudhuria hususan wale wanaotoka vijijini," alisema Kassiba.

Naye John Mwakipasile, mjasiriamali wa soko la Mwanjelwa, alisema maadhimisho hayo yamewaongezea uelewa wa fursa mbalimbali zinazopatikana katika sekta ya fedha.

Alisema katika maadhimisho hayo, wamepata ujuzi wa matumizi sahihi ya huduma za fedha katika kukuza biashara zao, utamaduni wa kujiwekea akiba, kukopa na kulipa madeni.

Maofisa Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Mbeya, nao waliishukuru serikali kwa kupeleka jijini Mbeya kwa kuwa yamewawezesha kuwapata wananchi wengi ndani ya muda mfupi.

Mratibu wa Mikopo wa Jiji la Mbeya, Aksa Njidile, aliwakaribisha wananchi kutembelea maadhimisho hayo, ili wapate elimu na huduma mbalimbali zinazotolewa.

Alisema wakitembelea katika maadhimisho hayo pamoja na mambo mengine, watapata elimu ya mikopo mbalimbali inayotolewa na serikali hususan ile ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri.

Naye Ofisa Vijana wa Jiji la Mbeya, Ritha Mushi, aliwahamasisha vijana wa jiji hilo kutembelea maadhimisho hayo, ili wapate elimu ya fursa mbalimbali za kujiinua kiuchumi zinazotolewa na serikali.

Maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa, yanatarajia kuongeza idadi ya watu wenye elimu ya fedha na maarifa juu ya upatikanaji na utumiaji wa bidhaa na huduma rasmi za kifedha pamoja na kuongeza mchango wa sekta ya fedha kwenye ukuaji wa uchumi.

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kesi ya kanga ilivyozaa mikopo kausha damu*



**Na Adam Fungamwangwo**

**Kwa sababu hana kipato, anaamua kukopa 'kausha damu' akitegemea kulipa kidogo kidogo kwa pesa za biashara ndogo kama kuuza karanga, maembe, ndizi, maandazi na chapati. Wakati mwingine**

HUKO mitaani hakulaliki. Kinamama wamekuwa wakikimbia nyumba zao, ili kuwakwepa watu kutoka kwenye taasisi zilizowakopesha. Taasisi nyingi ni zile ambazo hazitambuliwi na serikali.

Wamekuwa wakiwakopesha kinamama mikopo bila kufuata miongozo na kanuni za sheria za Benki Kuu ya Tanzania (BoT), huku wakiweka riba kubwa ambazo wengi wanashindwa kuzilipa.

Badala yake ikifika wakati wa kulipa, kinamama hawakai tena majumbani mwao. Wanahaha kukimbia na kwenda kushinda kwa ndugu na jamaa, ili kukwepa kuchukuliwa samani zao za ndani.

Tumeona au kusikia kwenye vyombo vya habari watu wanaowakopesha pesa kinamama wakivamia majumbani kwao na kubeba vitu vya ndani kama vile televisheni, friji, vitanda na vingine vinavyofanana na hivyo. Wanafanya hivyo kulipia zile pesa ambazo wamekopa na kushindwa kupeleka mrejesho.

Mikopo hii huko mitaani imepewa jina la kausha damu. Kinamama wamekuwa wakidhalilika sana na aina hii ya mikopo, kitu ambacho mara kwa mara kinaifanya serikali kuwatahadharisha kuhusu kukopa kwenye taasisi zisizo rasmi.

Wale ambao hawawezi kukimbia wamekuwa wakiuza vitu vya vya ndani kwa bei rahisi, ili mradi tu walipe pesa za watu kwani tayari wameshindwa kulipa kwa taratibu ambazo zilitakiwa awali.

Kuna baadhi ya kinamama wanakopa mikopo kausha damu, kwa sababu ya matatizo ya kifamilia kwa kuwa baadhi ya wanaume wanashindwa kutekeleza majukumu yao ya malezi ya nyumbani kwa familia, badala yake mzigo wote unamwelemea mama.

Kwa sababu hana kipato, anaamua kukopa 'kausha damu' akitegemea kulipa kidogo kidogo kwa pesa za biashara ndogo kama kuuza karanga, maembe, ndizi, maandazi na chapati. Wakati mwingine msingi unakata na kujikuta hana kitu.

Wako wanaokopa tu kwa sababu ya ufahari. Kutaka pesa ya kuanzisha sherehe, kutunzana na vitu vingine visivyo vya msingi kitu ambacho wakati mwingine haviwaletei wao tu matatizo, bali hata waume zao ambao wanalazimika kukomaa, ili vitu vya ndani vizichukuliwe na watu wao.

Wanawake wengine wanakopa bila hata waume zao kufahamu nini kinaendelea. Haya ni mambo ya 'kausha damu.' Michezo hii ya kukopa haikuanza miaka hii bali ilikuwapo hata zamani. Kingine ni kwamba wanaokopa wanawatia kwenye janga hata wale wadhamini ambao wanakwenda kutia saini, ili wapate mikopo ya pesa au vitu vingine.

Kuna kisa kimoja kilichosimuliwa na bendi ya Zaita Musica, wakakipa jina la "Kesi ya Khanga', kinachozungumzia juu ya dada mmoja aliyekwenda kumdhamini shoga yake, Monica, ili akope doti 10 za kanga.

Baada ya hapo Monica hakuonekana tena. Mdhamini akatiwa ndani, baadaye akatolewa kwa dhamana, mawili amtafute Monica ama yeye mwenyewe alipe au afikishwe mahakamani na hata kufungwa kifungo gerezani.

Dada wa watu akapata tetesi kuwa Monica alikimbilia Zambia, hivyo naye akaamua kumfuata, ili aje kupambana na kesi yake iliyomgeukia yeye. Wimbo huo uliotungwa na Freddie Ndala Kasheba kupitia bendi ya Zaita Musica, ulifyatuliwa mwanzoni mwa miaka ya 1990 ukaimbwa hivi;-

"Mama nipe nauli nikamtafute Monica, amekimbia Zambia na treni ya mizigo. Kisa cha kukimbia madeni yamemzidi, doti 10 za kanga alizokopa hajalipa. Anatafutwa na polisi popote apatikane na mimi rafiki yake nipo nje kwa dhamana. Nililala rumande siku mbili kituoni, usumbufu nilioupata kwa kweli sina raha."

Dada huyo anaomba nauli kwa mama yake amfuate Monica nchini Zambia, maana hali imekuwa mbaya, hali wala kulala kwa raha.

Naona bora niende Zambia nikamtafute Monica, nimlete Dar es Salaam, apambane na kesi yake. Oooh Monica, eee uko wapi eee."

Mdhamini huyo anaona bora tu amfuate na kumleta apambane na kesi yake vinginevyo, yeye ndiye atakayekuwa mjibuji.

"Mahakamani wameshapanga siku ya kusikiliza kesi, asipofika nitapelekwa jela kutumikia kifungo, ooh Monica, eee uko wapi eee."

Hapa unaona kwa nini bibie ameamua kulivalia njuga suala hili. Mshtakiwa asipofika, basi yeye mdhamini achague mawili, akatumikie jela au kulipa thamani ya doti 10 za kanga ambazo Monica alichukua.

Kifupi, hapa tunafundishwa kuwa makini na mikopo 'kausha damu', hasa kinamama pamoja na kuwa makini kuwadhamini watu wengine ambao si waaminifu. Wakikimbia wanakuachia, 'msala'.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanaume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. milioni 15, ili wamuachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

# Nyuma ya Pazia-6

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**


*****************************************

Kama ambavyo alitegemea, saa sita na nusu alisikia simu ikiita. Aliitegemea simu hiyo, ingawa ilimtisha. Alikuwa bado kwenye kochi akiwa anaangalia televisheni nyumbani kwake. Hakuwa na mke, kwani tangu alipoachana na Dora, mama Macaire, miaka miwili iliyopita akili yake haijakaa sawa. Walikuja hapo ni wanawake tu na kukidhi haja zake na kuondoka. Hakutaka kabisa hata wa sogea tukae, achilia mbali kuoa.

"Wewe mpumbavu unampenda mtoto wako kweli wewe?" Ilisikika sauti ile ambayo aliizoea, siyo ya jana iliyopigwa kule bondeni Kinondoni Mkwajuni.

"Tulikwambia usiwaeleze askari polisi kuhusu wewe kupeleka pesa kule. Ilikuwa ni siri yetu wawili kweli si kweli?"

"Kweli!" Akajibu kwa hofu. "Sasa ukafanya nini?" Ilikuwa ni sauti ya kufoka kwa hasira. "Unataka kumkosa mtoto wako?" "Hapana." "Halafu hizo pesa ni za polisi. siyo zako. Yaani unachukua pesa polisi, ili kutukamatisha? Si tulikwambia hizo fedha zitokane ni michango ya wanandugu wote? Kwa nini mkaenda kuchukua pesa za polisi. Unafikiri sisi wajinga? Yaani hatujui kuwa zile pesa tayari wameshazinakiri namba! Unataka tukamatwe."




Macky hakuwa na cha kusema bali kushangaa. "Ni kwa nini hawa watekaji wamejua kuwa pesa hizi zimechukuliwa kutoka hazina ya Jeshi la Polisi? Ina maana ndani ya jeshi kuna mtu anawapa siri hawa watekaji?" Akajiuliza mwenyewe.

"Sasa sikia. Tunakupa siku tatu, ukusanye kiasi hicho cha pesa. Safari hii siyo bonde la Kinondoni Mkwajuni tena. Ni bonde la Kigogo." "Kigogo wapi?" Macky akauliza kwa wasiwasi.

"Ukitoka Magomeni Mikumi kuelekea Kigogo. Kuna bonde pale ambalo hulima mbogamboga kabla ya kupandisha na kufika kwenye mzunguko wa makutano ya barabara ya Kawawa na Kigogo inayoelekea Mburahati na Mabibo.

Pale chini wanapolima bustani za mboga za majani kuna daraja. Tunataka uje ushuke na kuziweka kwenye uwazi wa daraja hilo la Kigogo. Nadhani umetuelewa." Macky alishusha pumzi na kukubali. "Sawa nimewasikia. Mtoto wangu yu hai lakini?" Akauliza. "Mtoto wako siyo tu yupo hai, lakini anaishi vizuri, kwa amani na raha tele kuliko hata alipokuwa anaishi huko. Huku anakula vizuri, analala vizuri, kila huduma anapata na anasoma tuisheni, ili masomo ya shuleni ambayo anayakosa sasa yasimpite. Wala sisi hatuna ubaya wa mtoto wala ugomvi na wewe, tunachotaka ni Sh. milioni 15 tu. Labda nikwambie kitu, hata zoezi hili litakapomalizika, tutakuwa na kazi kubwa ya kushawishi mtoto kurudi kwako kwa sababu atakataa. Anaishi vizuri kuliko alivyoishi huko, hivyo ondoa shaka..." "Basi naomba hata nisikie sauti yake." "Subiri kidogo." Sauti ilisikika na baada ya robo dakika ilisikika sauti. Ni sauti aliyoizoea ikiitwa "Baba, baba shikamoo..." baada ya hapo simu ikakatwa. Hakukuwa na mazungumzo mengine kutoka kwa mtoto wala kwa watekaji.

**Hilo lilimtia moyo na kuamua kumwambia kila kitu. Afande Chacha aliwatia moyo Macky pamoja na mzazi mwenzake Dora kuwa wasihuzunike, mtoto atapatikana.**

Awali, Macky alidhani ni dhihaka ya watekaji, lakini kwa mbali alianza kusadiki ya mtekaji aliyekua akizungumza naye. Sauti na mtoto wake ilionesha kuwa si mtu anayepitia kwenye shida au mateso kama ambavyo alikuwa anafikiria.

Hii haikuwa mara ya kwanza. Hata siku ya kwanza mtekaji alipomsikilizisha sauti ya Macaire, sauti yake ilikuwa ya uchangamfu. "Inawezekana ni kweli kuwa watekaji si watu makatili kama walivyoelezwa siku walivyonyakua kama kifaranga walipomteka. Wao wanachohitaji ni pesa tu. Na inawezekana ikawa ndiyo kazi yao. Ni wataalam wa kazi hizi. Wanachohitaji ni pesa, wala hawamkwazi, kumtisha wala kumtesa." aliwaza kwa sauti Macky.

Hata hivyo, kuna jambo lilikuwa likimtatiza pia. Ni kwa nini wakati mtoto wake anamwita kutaka kuongea naye hukatisha maongezi. "Leo ilikuwa ni hivi hivi kama siku zile ilikuwa hivyo hivyo, mtoto aliniita baba baba, lakini wakati akitaka kuendelea wakakatisha kwa kuzima simu. Ina maana hawataki niongee na mtoto wangu hadi mwisho? Hawataki kujua anaishishe?" Akajiuliza. Baadaye akajijibu mwenyewe. "Inawezekana wanaona kama ataniambia anaishi vizuri nitaona hakuna haja ya kuharakisha kutoa pesa."

***********************************

Afande Chacha alimbana Macky, mpaka akakubali maongezi ambayo aliongea na watekaji kwa mara ya pili.

Awali alikataa akidai hawajampigia tena simu. Afande Chacha hakukubaliana na hilo. Anawafahamu watekaji kwani si mara ya kwanza wala ya pili kuwa na kesi kama hiyo. Alijua ni lazima wabadilishe eneo. Na ni lazima wampigie kumtisha baada ya kutofanikiwa kwa zoezi la kwanza.

'Enhee wamekwambia safari hii ni wapi?" "Wamesema chini ya daraja la bonde la Magomeni Mikumi na Kigogo, upande wa kushoto kama unatokea Magomeni ambako kuna bustani za mbogamboga," alisema Macky, lakini akiwa na wasiwasi. "Mbona una wasiwasi sana?" "Afande mimi naogopa kwa sababu watekaji wameniambia mambo mengi ambayo yamenitisha. Wameniambia hizi pesa ni za polisi nilizowapelekea, hawazitaki kwa sababu zina namba ambazo mnazinakiri, hivyo mtawakamata hata kama wakifanikiwa kuzichukua. Wanataka ambazo ndugu tutachanga wenyewe. Na wameniambia kama nikiwaambia watamchinja mtoto wangu ni kuniambia tu sehemu ambayo maiti yake wataitupa." Hata hivyo afande Chacha alimhakikishia kuwa Jeshi la Polisi litatumia nguvu, ujanja, weledi na rasilimali zote walizonazo, ili kumwokoa mtoto kutoka mikononi mwa watekaji.

Hilo lilimtia moyo na kuamua kumwambia kila kitu. Afande Chacha aliwatia moyo Macky pamoja na mzazi mwenzake Dora kuwa wasihuzunike, mtoto atapatikana.

"Kama yupo hai kama ulivyosema na wewe mwenyewe umemsikia kwenye simu, basi hao nia yao ni pesa tu. Safari hii hatutochukua pesa za polisi. Kwa sababu za polisi ni mpya sana. Tutachukua kwa mtu mmoja hivi, atatuazima, tena tutachukua zile zilizochakaa ili wasijue kama zetu halafu utawapelekea. Kwa mara ya kwanza hatutatumia simu kuwasiliana kuhusu jambo hili, tumeitana hapa. Tumeamua pia kutomwambia Mwalimu Mkuu kuhusu hili suala. Ni kwa sababu mara ya kwanza habari zilivuja zinafika kwa watekaji. Safari hii tumeamua kama Jeshi la Polisi siri ibaki kwa wazazi na sisi polisi, ili tuone nini kitatokea. Siyo kama tunamtuhumu Mwalimu Kisanga, hapana, ila inawezekana kuna watu wa karibu anawafahamu anaongea nao, inaweza ikawa ndiyo watekaji, au wana uhusiano nao, maana utekaji umetokea huko kwenye shule yake." Afande Chacha aliwaambia wazazi hao jinsi walivyoamua kutovujisha siri.

"Na nyinyi msimwambie chochote kile kuhusu hili na siyo huyo tu mwalimu, msizungumze chochote kwa ndugu zenu na majirani, ili tuone jaribio la pili la kuwakamata watekaji kama litafanikiwa," alisema afande Chacha.

***Itaendelea Jumapili***



# JAYDEE AMWIMBISHA PROFESA JAY YA 'JOTO HASIRA' JUKWAANI

MKONGWE wa Bongo Fleva, Profesa Jay, amewapagawisha mashabiki wa muziki huo, pale alipopanda jukwaani kuimba wimbo wa 'Joto Hasira' akiwa na pamoja na Komandoo Lady Jaydee.

Komandoo Jaydee na Profesa Jay, walionekana kuutendea haki wimbo huo, baada ya kuimba kwa umahiri na kusababisha mashabiki waliojaa katika ukumbi wa Ware House, ulioko Masaki kushangilia kwa nguvu.

Tamasha hilo ambalo liliandaliwa na Komandoo Jaydee, lilihudhuriwa na idadi kubwa ya watu wakiwamo mastaa mbalimbali wa muziki, filamu na michezo.

# SHAKIRA BADO KANASWA

PAMOJA na kuwa na fedha nyingi na umaarufu, mwanamuziki wa Colombia, Shakira, amejikuta akiwa katika utumwa wa mapenzi kutokana na kushindwa kujikomboa baada ya kuachwa.

Shakira ameachana na aliyekuwa mume wake nyota wa zamani wa Barcelona, Gerard Pique na mara kadhaa ameonekana akitumia nyimbo zake kueleza hisia zake kutokana na tukio hilo.

Mama huyo wa watoto wawili, alitingwa na penzi la mwanasoka huyo na hata ilipofahamika wamechana, bado Shakira anaonekana hajakubaliana na matokeo, kiasi ambacho sasa analaumu maisha kwa kusababisha kumtenganisha na mume wake.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MAN UNITED YASAKA MAKOCHA

KLABU ya Manchester United tayari imefanya mazungumzo na makocha kadhaa miongoni mwao Xavi Hernandez na Ruben Amorim wa Sporting Lisbon, huku shinikizo la kocha wa sasa kuondoka likiongezeka. ***(Daily Mail)***

### DE BRUYNE KUTIMKIA MAREKANI

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Kevin de Bruyne mwenye umri wa miaka 33, anaweza kuhamia San Diego FC inayoshiriki Ligi Kuu ya soka ya Marekani, mkataba wa Mbelgiji huyo ukikamilika Juni mwakani. ***(GiveMeSport)***

### MORMOUSH APANGIWA BEI

KLABU ya Eintracht Frankfurt, imeweka thamani ya kati ya euro milioni 50 hadi 60 kwa mshambuliaji wa Misri, Omar Marmoush mwenye umri wa miaka 25, ambaye wawakilishi wake wamefanya mazungumzo na Liverpool. ***(Sky Germany)***

### ISAK AONGOZA KUTAKIWA ARSENAL

ARSENAL imeandaa orodha fupi ya washambuliaji wanaowawania na wenye viwango vya kimataifa, huku mshambuliaji wa Newcastle na Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 25, akiwa juu kwenye orodha hiyo. ***(TeamTalk)***

### CHILWELL KUTIMKIA WEST HAM

BEKI wa Chelsea, Ben Chilwell mwenye umri wa miaka 27, huenda akahamia West Ham huku Muingereza huyo akiendelea kutatizika kucheza chini ya Enzo Maresca. ***(Metro)***

### INTER MILAN YAMTAKA SANCET

INTER Milan, inavutiwa na kiungo mshambuliaji wa Athletic Bilbao, Oihan Sancet, mwenye umri wa miaka 24, ambaye pia amekuwa akihusishwa na Aston Villa. ***(Fichajes)***

### SPURS KUMUWEKEA NGUMU PORRO

KLABU ya Tottenham Hotspur, ina nia ya kumzuia beki wa Hispania, Pedro Porro mwenye umri wa miaka 25, kujiunga na Manchester City ambayo inamuona kama mbadala wa beki wa England, Kyle Walker, akiwa na umri wa miaka 34. ***(Football Insider)***

### LAMINE YAMAL AWANIWA ENGLAND

LIVERPOOL na Arsenal zinawania saini Lamine Yamal wa Barcelona mwenye umri wa miaka 17 kwani klabu hiyo ya LaLiga inaweza kulazimika kumuuza mshambuliaji wao chipukizi kutokana na matatizo ya kifedha. ***(TeamTalk)***

### RAPHINHA ALIFIKIRIA KUONDOKA

WINGA wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 27 amesema alifikiria kuondoka Barcelona zaidi ya mara moja katika misimu yake miwili ya kwanza na klabu hiyo na kutaka kujiunga na Man United. ***(ESPN)***

### MUNGUEZA KUMRITHI ARNOLD L'POOL

LIVERPOOL inapanga kumnunua mlinzi wa Celta Vigo, Oscar Mingueza mwenye umri wa miaka 25, kuchukua nafasi ya Trent Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 26. ***(Fichajes)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# CASTELLO LUKEBA KUTUA REAL MADRID

Mabingwa hao wa Hispania wanataka kuimarisha safu yao ya ulinzi na tayari wana.....

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid, imehusishwa na kutaka kumnunua beki wa kati wa RB Leipzig, Castello Lukeba huku wakiendelea kupima nani anafaa kwenye orodha yao ya wachezaji wanaowafuatilia, ili kuimarisha safu yao ya ulinzi.

Madrid msimu huu wamekuwa na mabeki watatu pekee wa kati, Antonio Rudiger, Eder Militao na Jesus Vallejo.

David Alaba ndiye beki wa kati pekee wa upande wa kushoto kwenye kikosi hicho, lakini amekuwa nje ya uwanja tangu Desemba mwaka jana, kutokana na jeraha la mguu na si suluhisho la muda mrefu kwa Madrid ikizingatiwa kwamba atSport imeripoti kuwa klabu hiyo imepiga hatua kadhaa katika harakati za kutafuta beki mpya, huku akiwamo kijana mwenye umri wa miaka 18, Vitor Reis wa Palmeiras.

Lakini Lukeba ana mguu wa kushoto na anakidhi vigezo ambavyo klabu inatafuta.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 alijiunga na RB Leipzig kutoka Lyon msimu wa majira ya joto wa 2023 na amecheza mechi tatu za Ligi ya mabingwa Ulaya hadi sasa msimu huu.

Lukeba, aliyeelezewa na wengine katika miezi ya hivi karibuni kama 'Josko Gvardiol ajaye', aliongeza mkataba wake hadi 2029, lakini kifungu cha kutolewa cha kuuzwa cha euro kadhaa.

HABARI MICHEZO

# GUARDIOLA: NIKIONDOKA MAN CITY, HAITAPOROMOKA

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola, amesema hakutakuwa na hali ya kuporomoka kwa kiwango kama Manchester United katika klabu ya Manchester City, iwapo ataamua kujiuzulu kama kocha, msimu ujao wa majira ya joto.

United haijashinda taji la Ligi Kuu England tangu Sir Alex Ferguson alipojiuzulu mwaka wa 2013.

City wameshinda katika kipindi cha miaka sita kati ya saba iliyopita na Guardiola amesisitiza kuwa, klabu hiyo itaendelea kushinda hata baada ya yeye kuondoka Etihad.

"Sijui ni nini kilitokea ndani ya Man United," alisema Guardiola.

"Itakuwa dalili mbaya kwa klabu ikiwa baada ya mtu mmoja tu kuondoka na kila kitu kinabadilika labda watafanya makosa, kisha makosa yatatatuliwa mara moja, hiyo ni hakika. Vijana wanajua nini wanapaswa kufanya," alisema Guardiola.

Kocha huyo raia wa Hispania mkataba wake wa sasa unamalizika mwisho wa msimu huu na hadi sasa hajaweka wazi kama ataongeza mkataba wake.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba City inatarajia kufanya uamuzi kati ya mapumziko ya kimataifa ya Novemba na mwaka mpya, ingawa wamekuwa wakifahamu kocha huyo wa miaka 53 atafanya uamuzi wake.

Mkurugenzi wa Soka wa klabu hiyo, Txiki Begiristain, tayari ameiambia klabu hiyo kwamba, ataondoka mwishoni mwa msimu huu na nafasi yake itachukuliwa na Hugo Viana kutoka Sporting Lisbon.

"Wao klabu watakuwa na subira, watulivu na wanajua wanachopaswa kufanya,

"Kweli kabisa sina mashaka na hilo, kwa Txiki kwa miaka 12 na kesi yangu ni jambo la kawaida kwamba naweza kuendelea, maisha yanasonga, dunia inaendelea," alisema Guardiola.

Aidha, alisema klabu hiyo inaendeshwa vizuri na muundo ni mzuri.

"Klabu imara haitegemei takwimu moja au nyingine. Klabu inapokuwa imara haijalishi. Vinginevyo haitakuwa nzuri," alisema Guardiola.



# PSG sasa kumpeleka Mbappe mahakamani

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya PSG itapeleka kesi yao ya mshahara na Kylian Mbappé mahakamani, baada ya Ligi Kuu ya Soka ya Ufaransa kutoa uamuzi unaomkinga nahodha huyo wa Ufaransa.

Vyombo vya habari vya Ufaransa viliripoti kwamba, Mbappé hajazungumza lolote kuhusu mzozo huo wa kulipwa takriban euro milioni 55, kama mshahara na marupurupu ambayo anaidaia klabu hiyo.

Mabingwa hao wa Ligue 1 wamesema mkataba wa Mbappé "ulirekebishwa kisheria" na kwamba alipuuza ahadi aliyoitoa kabla ya kwenda Hispania, kujiunga na Real Madrid wakati wa dirisha la usajili la majira ya kiangazi.

PSG ilisema mwezi uliopita kwamba Mbappé mwenye umri wa miaka 25, alikataa ofa ya kupatanishwa suala hilo.

Baada ya tume ya Ligi Kuu Ufaransa kusikiliza pande zote Oktoba 15, ilitangaza kwamba imeamua kumuunga mkono Mbappé.

"Klabu lazima imlipe mshahara anaodai. Uamuzi huu hauhitaji kukata rufani, lakini unaweza kupelekwa (Shirikisho la Soka la Ufaransa)," taarifa ya LFP iliambia Reuters.

Hata hivyo, PSG ilisema "italazimika kupeleka kesi hiyo kwenye mahakama zinazohusika" huku wakijaribu kukwepa kumlipa mchezaji huyo ambaye alikuwa mfungaji bora wa muda wote wa klabu hiyo.

"Kinachojadiliwa na hatimaye kitasikilizwa mbele ya mahakama inayofaa, ni kwamba mkataba wa awali una msimu wa 2024-25 na pia kutambuliwa kikamilifu kuvunja ahadi zake zote, baada ya kuondoka kwenye klabu," msemaji wa PSG alisema.

"Kama suala la sheria na ukweli, mchezaji ameweka wazi, mara kwa mara ahadi kwa umma na za kibinafsi, kwa sasa anapewa faida ambazo hazijawahi kutokea." ilisema PSG.

Januari mwaka huu, Mbappé alisema alifanya makubaliano na mwenyekiti wa PSG, Nasser Al-Khelaifi ambayo yangelinda pande zote.

# Szczesny: Sijacheza lakini nina furaha

**BARCELONA, Hispania**

WOJCIECH Szczesny, amesisitiza kuwa ana furaha kucheza kama kipa chaguo la pili mbele ya Inaki Pena wakati Barcelona "wanafanya kazi vizuri."

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Poland alistaafu kucheza soka, akiwa na umri wa miaka 34 kabla ya Barcelona kumrudisha tena uwanjani, baada ya jeraha la kipa Marc-Andre ter Stegen wakati wa mchezo dhidi ya Villarreal mwishoni mwa Septemba.


Szczesny alitambuliwa haraka kama mbadala wake na alilazimishwa kutoka kustaafu na kusaini mkataba wa msimu mmoja na Barcelona.

Licha ya kutegemewa na wengi kuchukua jukumu la kuwa kipa namba moja, Szczesny bado hajacheza hata dakika moja katika klabu hiyo, huku Inaki Pena akipendekezwa na Hansi Flick, kuwa chaguo la kwanza.

Akizungumza na Eleven Sports kuhusu kukosa muda wa kucheza huko Katalunya, mlinda mlango huyo wa Poland alikiri kwamba, anaelewa uamuzi wa Flick kutokana na kiwango kizuri cha sasa cha Barca.

"Inaki Pena hajampa sababu yoyote ya kumuacha benchi, tumezungumza mengi, tayari nimeshamwambia kocha kazi nzuri," alisema.

Barcelona imekuwa timu bora zaidi barani Ulaya, kwa sasa ipo kileleni mwa msimamo wa LaLiga wakiwa wameshinda kwa kushangaza mechi tisa kati ya 10 za kwanza na wiki hii ilipata ushindi wa Ligi ya Mabingwa kwa kuichapa Bayern Munich 4-1.



## HABARI MICHEZO

# STARS UGENINI KUIVAA SUDAN KUSAKA TIKETI FAINALI CHAN

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha timu ya soka ya Tanzania, Taifa Stars, leo saa 4:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki, kitajitupa kwenye Uwanja wa de la Capitale, jijini Nouakchott, nchini Mauritania kucheza mechi ya mtoano, kwa ajili ya kutafuta tiketi ya kucheza fainali za mataifa kwa wachezaji wanaocheza Ligi za ndani (CHAN), huku Kocha Mkuu, Bakari Shime akisema wapo tayari kwa mapambano.

Stars, inayoundwa na wachezaji wanaocheza hapa nchini, ipo chini ya kocha Shime, inacheza mechi hiyo nchini humo badala ya Sudan kutokana na nchi hiyo kuwa na machafuko ya vita kwa wenyewe kwa wenyewe.

Kocha Shime amesema kila kitu ambacho kinahitajika kwa ajili ya mchezo huo, kimefanyika na kinachosubiriwa ni wachezaji wake kuingia uwanjani, ili wakalipambanie taifa.

"Nawaamini vijana wangu, kuna watu wanasema wengi hawana uzoefu, ni kweli, lakini hawana uzoefu kwenye michezo ya kimataifa tu, lakini wana uzoefu wa kucheza kwenye klabu zao za Ligi Kuu, naamini wanaweza kwani hata wale ambao ni wazoefu walianza kama hawa," alisema Shime.

Kati ya wachezaji 24 walioteuliwa kuunda kikosi hicho, 11 wanatoka timu ya vijana chini ya miaka 20, Ngorongoro Heroes iliyotwaa Ubingwa wa CECAFA hivi majuzi nchini, kwa kuifunga Kenya mabao 2-1 katika mchezo wa fainali.

Kuhusu kipa Aishi Manula, alisema yeye atakuwa kama kocha wa ndani na ndiyo maana amemchukua kwenye kikosi hicho.

"Kwangu mimi kumchagua Manula nilichohitaji ni mdomo wake zaidi kuliko mikono yake,"

Hoja ni kwamba hajacheza muda mrefu, lakini Aishi yupo sawasawa, nafasi anayocheza ni ya golikipa na kama unavyoona wachezaji wote kwenye timu yetu wanaocheza nafasi ya ulinzi ni chipukizi, kwa hiyo wanamhitaji mtu nyuma yao ambaye anaweza kufanya kazi kama yangu mimi niliye kwenye benchi, namna gani anaweza kupeleka maelekezo sahihi na kuwafanya mabeki na wachezaji wote kucheza katika utaratibu unaotakiwa," alisema.

Baada ya mechi hiyo, timu hizo zitacheza mchezo wa marudiano, Novemba 3, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Fainali za CHAN zinatarajiwa kufanyika hapa nchini, Uganda na Kenya, kuanzia Februari Mosi hadi 28 mwakani.

# Azam, Singida BlackStars wanautaka ubingwa NBC

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya timu zao kupata ushindi kwenye michezo ya juzi, makocha wa Azam FC, Rachid Taoussi na wa Singida Black Stars, Patrick Aussems, wamesema msimu huu wanautaka ubingwa wa Tanzania Bara ambao kwa misimu 11 imekuwa ikihodhiwa na klabu za Simba na Yanga.

Wakizungumza mara baada ya mechi zao zilizochezwa Dar es Salaam na Singida, makocha hao wamesifu ushindani mkubwa uliopo msimu huu, wakisema itabidi timu za Simba na Yanga zifanye kazi ya ziada kama zinautaka ubingwa.

Juzi mchana kwenye Uwanja wa Liti Singida, Singida Black Stars ilimaliza dakika 90 na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Fountain Gate, mabao yakiwekwa wavuni na Josephat Banda dakika ya 54 na Ayoub Lyanga, dakika ya 65, ambayo yamezidi kuiweka timu hiyo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikifikisha pointi 22, ikiwa imecheza michezo minane, ikishinda saba na kutoa sare mmoja.

Usiku, kwenye Uwanja wa Azam Complex, Azam iliishindilia KenGold mabao 4-1 mabao yaliyowekwa kwenye kamba na Feisal Salum, Jhonier Blanco, Gibril Sillah na Cheikh Sindibe, huku la KenGold likifungwa na Joshua Ibrahim.

Ni matokeo yameifanya Azam kushika nafasi ya nne ikifikisha pointi 18, ikicheza michezo tisa na kuzidi kuweka shinikizo kwa timu za juu ya msimamo.

"Tuna furaha kwa ushindi kwa sababu tunazidi kupaa juu ya msimamo, nimekitengeneza kikosi na naona kimeanza kunipa kile ambacho nilikuwa nahitaji.

Nataka timu yangu icheze mpira wa kasi, wachezaji wangu wasikae na mpira sana, mara moja wameuachia, lakini pia wajitoe na kupambana, tukifanya hivi tunaweza kutwaa ubingwa ambao upo wazi, yoyote anaweza kuchukua, hata sisi msimu huu kwa kikosi hiki tunaweza kuupata," alisema Taoussi.

Naye Aussems amesema ushindi wanaopata ni kielelezo tosha kuwa wanataka kufanya mabadiliko kwenye nafasi ya juu msimu huu.

"Tumeongoza ligi kwa kipindi kirefu, nia yetu ni kukaa pale mpaka mwisho ingawa si rahisi, lakini tunataka kule juu kuwe na mabadiliko," alisema.




Naibu Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma (katikati), akisikiliza maelezo juu ya udhamini wa Korosho Marathon 2024 kutoka kwa Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Pwani Vijijini, Aidan Komba (kulia), mwingine ni Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mjini, Abdallah Mwaipaya. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## Yanga inapiga kila inayemkuta

INATOKA UK. 24

cha Maabad Maulid, kugonga nguzo ya chini pembeni kulia kwa kipa, Khomeiny.

Ilikuwa ni krosi ya Ernest Malonga aliyoipiga kutoka upande wa kulia na kwenda kutua kichwani mwa mshambuliaji huyo na kuzua kizaazaa na wachezaji wa Coastal miguu yao ilionekana kuwa na kigugumizi kuukwamisha mpira wavuni.

Dakika ya 23, Coastal, ambayo karibu muda mrefu ya kipindi cha kwanza walicheza nyuma ya mpira, walirejea tena langoni mwa Yanga.

Alikuwa Maabad tena akiwa kwenye nafasi nzuri, akapiga shuti kali la chini akiwa nje ya eneo la hatari, lakini mpira uliishia mikononi mwa kipa Khomeny.

Kwa kiasi kikubwa kipindi cha kwanza hakikuwa cha kuvutia sana kutokana na Yanga kutocheza mpira wao wa kasi ambao umezoeleka, badala yake ilikuwa ikicheza taratibu, pasi fupi fupi na mara moja moja mabeki wakipiga pasi ndefu pembeni.

Angalau kipindi cha pili mpira ulichangamka hasa baada ya Yanga kuwaingiza Prince Dube, Clatous Chama, Pacome Zouzoua, Duke Abuya na Aziz Andambwilem kuchukua nafasi za Beleke, Nzengeli, Stephane Aziz Ki, Yao Kouassi aliyeumia na Clement Mzize.

Coastal Union walikaribia kufunga, lakini Gerson Gwalala alikosa bao la wazi dakika ya 71.

Pacome naye alishindwa kupachika bao dakika nane kabla ya mpira kumalizika, baada ya kuwalamba chenga mabeki watatu wa Coastal Union, huku Dube naye akikosa dakika moja kabla ya mpira kumalizika.

## Fadlu apagawa viwango wachezaji

INATOKA UK. 24

Mutale ambacho alisema kilikuwa cha hali ya juu na kuwapa tumbo joto wapinzani kila alipokuwa akigusa mpira na kuamua kumchezea madhambi mara kwa mara.

"Hii inanipa wakati mzuri wa mimi kama kocha kuwa na machaguo mapana, kila mchezaji sasa anatakiwa kuonyesha kiwango chake, kila mchezaji anatakiwa kutoa mchango kwenye kikosi hiki kwa ajili ya kupata mafanikio," alisema.

Wakati Fadlu akipagawa na viwango vya wachezaji wake, Kocha msaidizi wa Namungo, Ngawina Ngawina, ambaye aliendelea kukaa benchini kama Kocha Mkuu, huku Juma Mgunda aliyetangazwa juzi akiwa jukwaani, alikiri kuzidiwa mbinu na wapinzani wake, huku akiwapongeza kwa ushindi huo.

"Tumepoteza mchezo tuwapongeze wapinzani wetu, wamepata pointi tatu ambazo wanastahili, tumefungwa kwa sababu mipango yetu haikufanya kazi, tulivyokuja kucheza tulijua ubora wao tulijaribu kukaa nyuma kwanza, lakini tukaruhusu bao la mapema kila kitu kikaharibika ilibidi tutoke nyuma, mfumo wote ukaharibika," alisema Ngawina.

# Michezo



Jumapili Oktoba 27, 2024

Nipashe

## Castello Lukeba kutua Real Madrid

UKURASA 21

# Fadlu apagawa viwango wachezaji

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya juzi kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Namungo FC, kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, ameonekana kufurahishwa na viwango vya wachezaji wake licha ya kwamba alifanya mabadiliko ya kikosi kwa kiasi kikubwa.

Fadlu, raia wa Afrika Kusini, alisema alitarajia kuwa wachezaji wake watacheza soka safi, lakini si kwa kiasi ambacho amekiona katika mchezo huo, huku akipagawa na uwezo wa baadhi ya wachezaji ambao wamekuwa hawaanzi mara kwa mara.

Katika mchezo wa juzi, kocha huyo aliwaanzisha wachezaji ambao huwa hawapati sana nafasi ya kucheza kama Chamou Karaboue, Velentine Nouma, Fabrice Ngoma, Agustine Okejepha, Steven Mukwala, Awesu Awesu na Ladack Chasambi ambao waliwashangaza mashabiki wa Simba waliojazana kwenye uwanja huo kwa kuonyesha kiwango cha hali ya juu.

"Ulikuwa ushindi muhimu baada ya ule wa Mbeya dhidi ya Prisons, tumepumzika siku mbili tu kabla ya mchezo huu.

Ulikuwa ni wakati mzuri wa kumuona Valentino Nouma akirejea dimbani baada ya muda mrefu, nimefanya mabadiliko kwenye kikosi ili kuwapumzisha baadhi ya wachezaji kwani wamecheza michezo mingi, wamenishangaza kwa kweli, Ngoma alikuwa kiongozi mzuri uwanjani, Okejepha angeweza kuwa mchezaji bora wa mechi, Mukwala ameonyesha kiwango cha juu na kusababisha mabao mawili, Awesu, alikuwa kwenye kiwango bora bahati mbaya akaumia, Chasambi alikuwa hatari mno pale mbele kwa wapinzani," alisema kocha huyo.

Fadlu pia alionekana kufurahishwa na kiwango cha Joshua

INAENDELEA UK 23




Kiungo wa Yanga, Aziz Ki (kulia), akimtoka mchezaji wa Coastal Union, Miraji Hassan, kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa jana, Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# YANGA INAPIGA KILA INAYEMKUTA NJIANI

## ●●●Yachomoza na ushindi mbele ya Coastal Union, sasa yafikisha.....

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, jana wameendeleza ushindi wao wa asilimia 100 baada ya kuifunga Coastal Union bao 1-0 katika mchezo uliochezwa, Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha.

Lilikuwa bao pekee lililofungwa na mshambuliji raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Jean Baleke, lililoipa Yanga ushindi na kufikisha pointi 21, ikiiengua Simba katika nafasi ya pili kwenye msimamo.

Yanga pia imeendeleza rekodi yake ya kutoruhusu bao lolote nyavuni kwake mpaka sasa, licha ya jana kutokuwapo kwa kipa namba moja, raia wa Mali, Djigui Diarra, badala yake alisimama, Khomeiny Aboubakar aliyesajiliwa mwanzoni mwa msimu huu akitokea, Singida Black Stars.

Maxi Nzengeli

Kipa huyo pia ameingia kwenye rekodi ya kupata 'clean sheet' moja, huku mwenzake akiwa nazo sita.

Kona iliyopigwa na Maxi Nzengeli dakika ya 25 iliwachanganya mabeki wa Coastal Union ambao walikosea kuuokoa na kuendelea kuzagaazagaa langoni kiasi cha kutokea purukushani, kabla ya Baleke kuukwamisha mpira wavuni.

Bao hilo ni la kwanza kwa Baleke msimu huu, kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara tangu asajiliwe akitokea klabu ya Al Ittihad ya Libya.

Matokeo hayo yanaifanya Yanga kucheza michezo saba, ikishinda yote na kufikisha mabao 12 kibindoni, ikiwa nafasi ya pili pointi moja nyuma ya Singida Black Stars iliyo kileleni kwa pointi 22.

Hata hivyo, Singida imecheza michezo minane, hivyo iko mbele mchezo mmoja nyuma ya mabingwa hao watetezi.

Coastal ilianza kulisabahi lango la Yanga dakika ya tisa ya mchezo, kwa shambulizi la kushtukiza ambalo lingeweza kuwapatia bao kama si mpira wa kichwa

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002